Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

# YAKOBO

**na**

**Jonathan M. Menn**

**Kimetafsiriwa na**
**Michael D. Nyangusi**

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974**
**J.D., Cornell Law School, 1977**
**M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders East Africa, Inc.**
**714 S. Summit St., Appleton, WI 54914**
**+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)**
**jonathanmenn@yahoo.com**
**www.eclea.net**

2019

Kitabu hiki cha Yakobo huenda kiliandikwa na ndugu wa kambo wa Yesu, na wanazuoni wengi wanafikiria pengine hiki ndicho kitabu cha kwanza kuandikwa katika Agano Jipya. Kitabu hiki kina mifano mingi inayofanana na ile ya mafundisho ya Yesu. Kitabu hiki kinakazia kuhusu yale ambayo ni lazima ili sisi tuishi kama tunavyopaswa. Kinajadili mengi kati ya yale ambayo ni mambo muhimu zaidi ya maisha, ni pamoja na: majaribu, vishawishi, na matamanio; maombi; dhambi ya upendeleo; asili ya imani ya kweli, iliyo hai; kuutawala ulimi; hekima ishukayo kutoka juu dhidi ya hekima isiyotoka juu; dhambi ikaayo ndani na udhihirisho wake wa nje; dhambi ya kujitawala na udhihirisho wake wa nje; na uaminifu wa kweli.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

## YALIYOMO

**I. Utangulizi……………………………………………………………………………………..2**

**II. Yak 1:1-27—Utangulizi wa mada zote kuu…………………………………………………………..3**

**III. Yak 2:1-13—Dhambi ya upendeleo…………………………………………………………......12**

**IV. Yak 2:14-26—Imani iliyo hai/inayotenda kazi…………………………………………………....16**

**V. Yak 3:1-12—Dhambi ya kutotawala ulimi……………………………………………………………20**

**VI. Yak 3:13-18—Hekima itokayo juu dhidi ya ile isiyotoka juu………………………………………....23**

**VII. Yak 4:1-4—Dhambi iliyo ndani na madhihirisho yake ya nje……………………………………..23**

**VIII. Yak 4:5-10—Jinsi ya kuitafuta neema ya Mungu na kupata hekima kutoka juu…………………26**

**IX. Yak 4:11-5:6—Dhambi ya kujitawala na madhihirisho yake ya nje………………………………….27**

**X. Yak 5:7-20—Nasaha za kuhitimisha…………………………………………………………………..30**

**BIBLIOGRAFIA……………………………………………………………………………………...35**

**MWANDISHI………………………………………………………………………………………….36**

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

# I. Utangulizi

## A. *Mwandishi*

Kitabu cha Yakobo kinadai kuwa kimeandikwa na *"Yakobo, mtumwa wa Mungu, na wa Bwana Yesu Kristo"* (**Yak 1:1**). Carson na Moo wanasema kwamba "kukosekana kwa maelezo zaidi husababisha mwelekeo uwe kwa Yakobo anayejulikana zaidi" (Carson na Moo 2005: 621). Watu waliojulikana zaidi wenye jina hilo katika Biblia na katika kanisa la kwanza walikuwa ni mtume Yakobo na Yakobo ndugu yake Yesu. Mtume Yakobo aliuawa karibia na mwaka 44 BK, kipindi hicho kilikuwa mapema sana kwa barua yenyewe. Kwa hivyo mwandishi ambaye anaweza kuwa ndiye hasa ni Yakobo ndugu yake Yesu, huu ukiwa ndio mtazamo wa kimapokeo na mtazamo wa wanazuoni walio wengi wa kibiblia (Eusebius 1988: 78-79 [*Ecclesiastical History* 2.23.25]; Carson na Moo 2005: 621-26). "Kuthibitisha uamuzi huu ni mfanano wa kushangaza kati ya Kiyunani cha Waraka wa Yakobo na kile cha hotuba inayodhaniwa kuwa ni ya Yakobo katika Matendo 15:13-21" (Carson na Moo 2005: 622).[1]

## B. *Kipindi cha uandishi*

Ingawaje bado kuna mabishano kuhusu lini kitabu kiliandikwa, ni wazi kwamba ni kitabu cha AJ kilichoandikwa mapema. Harold Lindsell anataarifu, "Ikiwa utambulisho wa kimapokeo wa mwandishi uko sahihi, waraka huu unaweza kuwa umeandikwa kabla ya mwaka 62 BK, kipindi ambacho Yakobo aliuawa. Wengine wanashikilia kwamba kilikuwa kitabu cha kwanza cha Agano Jipya kuandikwa, mnamo mwaka 45 BK." (Lindsell 1971: 1822) Wanazuoni wengi wanaokubali kwamba Yakobo ndugu yake Yesu ndiye mwandishi huhitimisha kwamba kitabu hiki kiliandikwa mnamo miaka ya kati ya 40 BK, kabla ya baraza la Yerusalemu la Matendo 15 ambalo lilifanyika mwaka 49 BK au 50 BK (angalia Carson na Moo 2005: 627; *Africa Study Bible, New Living Translation* 2016: 1841; *Life Application Study Bible, New International Version* 1986: 2243; *New American Standard Bible* 1995: 1159).

## C. *Kufanana kwake na mafundisho ya Yesu*

Kuna kufanana kwingi kuliko dhahiri kati ya Yakobo na mafundisho ya Yesu, hasa kama ilivyoandikwa katika Mathayo na Luka. Katika matukio mengine kuna kufanana kuliko wazi katika matamshi:

| Yakobo | Mathayo | Luka | Somo |
|---|---|---|---|
| 1:2 | 5:12 | | kufurahi katika majabribu |
| 1:4 | 5:48 | | kuwa wakamilifu |
| 1:5; 4:2-3 | 7:7 | 11:9 | omba na utapewa |
| 1:12 | 5:11-12; 24:13 | 6:22-23 | kustahimili dhidi ya majaribu |
| 1:19-20 | 5:22 | | dhidi ya hasira |
| 1:22-25; 2:14-17 | 7:24-27 | 6:46-49; 11:28 | kuwa watendaji wa Neno |
| 2:5 | 5:3 | 6:20 | ufalme ni wa maskini |
| 2:8 | 22:36-40 | 10:25-28 | kumpenda jirani wako |
| 2:13 | 5:7 | | matokeo ya rehema |
| 3:12 | 7:16-18 | 6:44 | tunda la mti |
| 3:18 | 5:9 | | kuwa wapatanishi |
| 4:4 | 6:24 | 16:13 | dhidi ya kuwa na nia mbili mbele za Mungu |
| 4:8 | 5:8 | | usafi wa moyo na ukaribu na Mungu |
| 4:9 | | 6:21, 25 | wale wanaocheka wataomboleza |
| 4:10 | 23:12 | 14:11; 18:14 | wanyenyekevu watainuliwa |
| 4:11-12 | 7:1-2 | 6:37 | dhidi ya kuwahukumu wengine |
| 5:1 | | 6:24 | ole kwa matajiri |
| 5:2-3 | 6:19-20 | 12:33 | msilundike mali nyingi |
| 5:9 | 24:33 | | hakimu yuko mlangoni |
| 5:12 | 5:33-37 | | kiapo: ndiyo yenu iwe ndiyo na siyo yenu iwe siyo |

## D. *Muhtasari*

Waandishi tofauti wamependekeza muhtasari mbali mbali wa kitabu cha Yakobo kutokana na mitazamo yao kuhusu dhamira na muundo wa kitabu (angalia Martin 1988: xcviii-civ). Yakobo kina muundo unaoweza kutambulika. Misemo mifupi, yenye maana sana (mithali, maneno ya hekima) ya sura ya 1 imefafanuliwa katika sura zinazofuata.[2] Sura 2-5, angalau katika namna ya ujumla, ziko katika mpangilio uliogeuzwa wa misemo ile

---

[1] Kwa mambo zaidi kuhusu utambulisho wa Yakobo, angalia mjadala hapo chini katika **Yakobo 1:1**.

[2] "Sura ya kwanza inatenda kazi kama kitu kinachofanana na 'yaliyomo' tasnifu, au 'mazungumzo ya awali' ya mada zake"

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

iliyo katika sura ya 1 kwa ile inayokubaliana. Kilele cha kitabu kinachokamilisha ni **3:13-18**, "hekima itokayo juu," ambayo ndiyo iliyo ya lazima kwa ajili yetu sisi kuishi kama tunavyopaswa. Zaidi ya hayo, kitabu hiki kinatumia mfululizo wa tukio moja baada ya jingine ambayo huonyesha tofauti iliyopo kati ya njia chanya za namna tunavyopaswa kuishi na njia hasi (za dhambi) ambazo ndizo mwelekeo wetu wa kuishi. Kwa hiyo, muhtasari wa kitabu hiki waweza kuwa kama ifuatavyo:

**1:1-27**—Utangulizi wa mada zote kuu: chanya
- Mtumaji na anwani (1:1)
- Kujaribiwa, majaribu, na vishawishi (1:2-4, 12-15)
- Hekima, neema na maombi (1:5-8, 16-18)
- Matajiri na maskini (1:9-11)
- Ulimi (1:19-20, 26)
- Uaminifu wa kweli (1:21-27)

**2:1-13**—Dhambi ya *upendeleo* (angalia 1:9-11): hasi

**2:14-26**—*Imani* iliyo hai/inayotenda kazi (angali 1:22-27): chanya

**3:1-12**—Dhambi ya *kutotawala ulimi* (angalia 1:19-20, 26): hasi

**3:13-18**—*Hekima itokayo juu dhidi ya* hekima isiyotoka juu (angalia 1:5-8, 16-18): chanya

**4:1-4**—*Dhambi iliyo ndani* na madhihirisho yake ya nje: magonvi; migogoro; vita; mauaji; zinaa, ina maanisha, ishara ya kwamba *huna* hekima kutoka juu (angalia 1:13-15): hasi

**4:5-10**—Jinsi ya *kuitafuta* neema ya Mungu na *kupata* hekima kutoka juu (angalia 1:2-4, 12): chanya.

**4:11-5:6**—Dhambi ya *kujitawala* na madhihirisho yake ya nje: kuhukumu; kiburi; na tamaa ya vitu, ina maana, ni ishara kwamba *hujajinyenyekesha* au kujitiisha kwa Mungu (angalia 1:9-11, 14-15, 20-21): hasi

**5:7-20**—Nasaha za kuhitimisha ambazo huzungumzia tena mada zile kuu, ispokuwa ile ya matajiri/maskini, ambayo ilishughulikiwa katika 5:1-6: chanya
- Kujaribiwa, majribu, na vishawishi—5:7-11, 13 (see 1:2-4, 12-15)
- Ulimi—5 :9, 10, 12, 16 (angalia 1:19-20, 26)
- Maombi—5:13-18 (angalia 1:5-8)
- Uaminifu wa kweli—5:19-20 (angalia 1:21-27)

## II. Yak 1:1-27—Utangulizi wa mada zote kuu

***1:1—Yakobo, mtumwa wa Mungu, na wa Bwana Yesu Kristo, kwa kabila kumi na mbili waliotawanyika; salamu.***

***"Yakobo, mtumwa wa Mungu, na wa Bwana Yesu Kristo."*** Tukiwa tunaamini kwamba Yakobo ndugu yake Yesu ndiye aliyeandika waraka huu, tunajua mambo kadhaa muhimu kuhusu yeye:
- Jina lake halisi ni Yakobo (ndivyo inavyoandikwa kwa Kiyunani AJ); Likawa Yakobo kutokana na tafsiri katika lugha mbali mbali za Ulaya.
- Yeye alikuwa mmoja wa ndugu wa kambo wa Yesu (**Math 13:53-55; Marko 6:3; Gal 1:19**), huenda alizaliwa baada ya Yesu kwa sababu yeye ameandikwa wa kwanza katika **Math 13:55** na **Marko 6:3**.[3]

---

(Johnson 1995: 15). Ralph Martin vivyo hivyo anaandika, "Sura ya 1 ndiyo ufunguo wa muundo wa waraka huu na huweka wazi swala la msingi linalotakiwa kukabiliwa: namna ambavyo watu katika kuishi wanaweza kutekeleza malengo na kuyapatia heshima?" (Martin 1988: cii).

[3] Mara kwa mara Biblia inasema kwamba Yesu alikuwa na angalau ndugu wa kiume wanne (Yakobo, Yusufu, Simoni, na Yuda wametajwa) na angalau madada wawili (angalia **Math 12:46-47; 13:53-56; Marko 3:31-32; 6:3; Luka 8:19-20; Yohana 2:12; 7:3, 5, 10; Matendo 1:14; 1 Kor 9:5; Gal 1:19**). Kwa sababu ya mtazamo wa kwamba Mariamu alidumu kuwa bikira, Wakatoliki wanashikilia kwamba ndugu wa Yesu walikuwa binamu zake. Hata hivyo, "kifungu pekee ambapo

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Yeye pia ni kaka wa Yuda, mwandishi wa waraka wa Yuda (**Yuda 1**; angalia pia **Math 13:55** [kwa Kiyunani Yuda ni "Judas").

- Wakati wa huduma ya Yesu duniani akiwa katika mwili, Yakobo na ndugu zake wengine hawakumwamini (**Marko 3:21; Yohana 7:5**). Hata hivyo, Yakobo alibadilishwa wakati Yesu alipomtokea baada ya kufufuka kwake (**1 Kor 15:7**).
- Yakobo alikuwepo pamoja na wanafunzi katika chumba kile cha juu siku ile ya Pentekoste (**Matendo 1:14**) na akawa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu (**Matendo 12:17**); alikuwa na nafasi maalumu katika Baraza muhimu la Yerusalemu, inavyoonekana alikuwa ndiye mwenyekiti wa Baraza na ndiye aliyekuwa akitangaza maamuzi ya Baraza (**Matendo 15:13-29**). Alijulikana kama mmoja wa "nguzo" za kanisa (**Gal 2:9**).
- Sifa za Yakobo ziliongezeka, na akatambulika kama "Yakobo mwenye haki" (Eusebius 1988: 76 [*Ecclesiastical History* 2.23.4, 7]).
- Aliuawa mnamo mwaka 62BK kwa kupigwa kwa mawe hadi kufa baada ya kusukumwa kutoka kilele cha mnara mrefu wa hekalu (Eusebius 1988: 77 [*Ecclesiastical History* 2.23.11-16]; Josephus 1987, *Ant.:* 20.9.1).

***"Kwa makabila kumi na mbili waliotawanyika."*** Yakobo ni Mkristo (**Yak 1:1; 2:1**) na anawaandikia Wakristo (angalia **Yak 5:14** na anavyosema kuhusu kuwaita *"wazee wa kanisa"*). Hata hivyo, Yakobo alilelewa kama Myahudi na alikuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu. Kwa kuzingatia kweli hizi, kuna mitazamo miwili mikuu kuhusiana na *"makabila kumi na mbili waliotawanyika"* kuwa wao ni nani: Wakristo wa Kiyahudi waliokuwa wakiishi nje ya Palestina, au Wakristo wote (Wayahudi na Wamataifa).

1. <u>Wakristo wa Kiyahudi waliokuwa wakiishi nje ya Palestina.</u> Kuna sababu ambazo huonyesha kwamba walengwa wa waraka huu walikuwa Wakristo wa Kiyahudi waliokuwa wakiishi nje ya Palestina.
    - **Matendo 11:19** inavyoonekana huzungumza kuhusu Wakristo wa Kiyahudi ambao walikuwa "wametawanyika" nje ya Palestina. In **Yak 1:1** neno "waliotawanyika" (*diaspora*) kwa Kiyunani ni kitenzi cha neno "tawanya" katika Matendo. Ndivyo kwa namna hiyo *diaspora* inatumika katika **Yohana 7:35**.
    - Wakati **Yak 2:2** inapozungumzia kuhusu "kusanyiko" la Wakristo, neno halisi lililotumika ni "sinagogi."
    - Katika kitabu chote, Yakobo hutumia mifano ya AK, sitiari na dokezo ikimaanisha kwamba wasomaji wake walikuwa wajuzi wa AK.
2. <u>Wakristo wote (Wayahudi na Wamataifa).</u> Sababu nyingine hupendekeza kwamba walioandikiwa wa msingi walikuwa Wakristo wote, bila kujali kama asili yao ni Wayahudi au watu wa Mataifa.
    - "Mababila kumi na mbili" haimaanishi kwamba hawa walikuwa Wakristo wa Kiyahudi lakini inaonyesha kwamba "mwandishi anawatazama wapokeaji wa waraka kama Israeli wa kweli. Kimsingi kanisa kwa namna iliyo ya kiasili lilikuwa limejitwalia jina hilo la heshima, kwa kuwa ilikuwa ni kazi ya Masihi kuyarejesha upya makabila kumi na mbili (Yer. 3:18; Ezk. 37:19-24; Pss. Sol. 17:28), na Wakristo walitambua kwamba wao walikuwa warithi halisi wa imani ya Kiyahudi (Warumi 4; 1 Kor. 10:18; Gal. 4:21-31; Fil. 3:3)." (Davids 1982: 63; angalia pia Moo 1985: 58)[4]
    - Neno *diaspora* ("waliotawanyika") vile vile "lilikuwa na maana ya sitiari, kwa kuchukulia Wakristo kiujumla kama wale ambao huishi mbali na makao yao halisi ya mbinguni (1 Petro 1:1)" (Carson na Moo 2005: 628; angalia pia **Ebr 11:13; 13:14; 1 Pet 1:17; 2:11**).
    - Matumizi ya mifano ya AK, sitiari na dokezo si jambo geni, kwa kuwa waandishi wote wa kibiblia hutumia taarifa kutoka katika AK kwa kuwa AK ndio msingi kwa ajili ya AJ. Hata

---

ndugu wa Yesu hawakuunganishwa na mama yake ni Yohana 7:3, 5, 10. Muunganiko uliotajwa wa mama wa Yesu unaonyesha ni watoto wa mama mmoja." (Zodhiates 1993: *"adelphos,"* 80) Zaidi ya hayo, ukweli kwamba Yesu alikuwa mkubwa wa "ndugu" halisi (sio binamu) "unategemezwa na kama inavyoonekana maana ya 'mzaliwa wa kwanza', *prōtotokos,* katika Lk. ii. 7. Haitegemewi kama Luka angetumia neno hili, kama angejua kama Mariamu hakuzaa watoto wengine, kwa lile neno *monogenes* (lililotumika katika Lk. vii. 12, viii. 42 wa 'pekee' watoto) amelazwa tayari. Pia tunapaswa kutambua kwamba maana ya asili ya maneno katika Mt. i. 25 'asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe akamwita jina lake Yesu' ni kwamba, taratibu za kawaida za mahusiano ya kindoa ziliendele na watoto wengine walizaliwa." (Tasker 1982: 22-23)

[4] Kristo na kanisa katika kulitimiza AK na kulianzisha jipya, la kweli, Israeli waaminifu wanajadiliwa kwa kina katika Menn 2016: 26-93.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

matumizi ya "sinagogi" katika **Yak 2:2** maana yake sio lazima iwe mkutano wa Wakristo wa Kiyahudi, kwa kuwa katika **Ufu 2:9** na **3:9** Yesu anatumia neno hilo wakati akisema na kanisa kwa ujumla.

- "Ikiwa makabila kumi na mbili' lazima wawe Israeli wa asili, basi itakuwa haieleweki ni kwa namna gani iwahusu Wayahudi tu ambao wamekuwa Wakristo [kwa kuwa hakuna ambacho kinasemwa kuhusu yale 'makabila kumi na mbili' kuwa Wakristo]. Mantiki inadai kwamba ama tulielewe hilo neno kuwa linawahusu Wayahudi wote tu, au vinginevyo tulielewe neno hilo kwa namna ya ishara." (Nystrom 1997: 38) Kwa kuwa muktadha wa kitabu chote uko wazi kwamba kimepelekwa kwa Wakristo, sio Wayahudi, wale "kabila kumi na mbili" lazima wawe ni ishara au wa sitiari inayolielezea kanisa kiujumla, si kama kundi lenye misingi ya kikabila ambalo ni sehemu ya kanisa lote.
- Ujumbe wa Yakobo unafaa kwa ajili ya Wakristo wote wa vizazi vyote kila mahali. Ukweli ni kwamba hakuna cho chote katika ujumbe wa Yakobo—ama wazi wazi au kwa kudokeza—ambacho kinalenga tu Wakristo wa Kiyahudi dhidi ya Wakristo wa Mataifa. Badala yake, kitabu chote kinafaa kwa ajili ya Wakristo wote, bila kujali wapi wapo na asili yao kikabila. Hii hutiririka kutoka kwenye ukweli kwamba, ndani ya Kristo, *"hapana Myahudi wa Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wa mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu"* (**Gal 3:28**; angalia pia **Kol 3:11**). Kitabu hiki ni chanzo kizuri cha hekima na cha kimatendo kwa ajili ya waamini wa kila mazingira.

**1:2-4—**[2] ***Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali;*** [3] ***mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi.*** [4] ***Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.***

Yakobo anaanza kiini cha waraka wake kwa kuibua moja ya maswala muhimu ambayo sote tunakutana nayo: kujaribiwa kwa imani yetu kwa njia ya majaribu na vishawishi tunadumu na kuimarika na kwa namna tunavyoyachukulia. Kuna mambo kadhaa muhimu yahusuyo swala hili ambayo yamegusiwa katika mistari hii.

1. Neno la Kiyunani ambalo limetafsriwa kama neno "majaribu" (*peirasmos*) linaweza pia kutafsiriwa kama "vishawishi." Zodhiates anaelezea tofauti yake: "Jaribu, vishawishi, huweka katika kupima, ikiwazungumzia watu tu. Mhusika anapokuwa ni Mungu, kusudi la *peirasmos* ni kumthibitisha mtu, na kamwe si kwa kusudi la kumfanya aanguke. Ikiwa ni shetani anayejabu, basi hapo ni kwa kusudi la kumfanya mtu aanguke." (Zodhiates 1993: *"peirasmos,"* 1135) Marshall, Travis, na Paul wanafafanua hivi: "'Majaribu' tutayoyasema si lazima yawe ni mateso ya wazi wazi, lakini ni aina yoyote ya mgandamizo wa mawazo ambao unamjaribu mwamini kuiacha imani, kwa mfano maradhi, au msiba, usumbufu wa majirani wasioamini, ugumu wa kuishi kwa kufuata maadili ya Kikristo katika dunia yenye upinzani. Majaribu hayo si mitego ambayo imewekwa na Mungu kwa ajili yetu, lakini inaweza kutoka kwenye asili yetu ya ubinadamu au kutoka kwa shetani (1:13-16; 4:7). Lakini kuweza kustahimili majaribu ya namna hiyo hutuongeza katika kukua kiroho kuelekea ukomavu na hatimaye kufikia kushinda 'taji ya uzima' (1:4, 12; 5:7-11)." (Marshall, Travis, na Paul 2002: 257)
2. Muktadha wa **mst.2-4** inaonyesha kwamba tafsiri iliyo sahihi hapa ni "majaribu." Hili huonekana tunapoangalia *mwenendo* wetu wakati wa magumu na majaribu tunayokutana nayo na yale *matokeo* ya kustahimili mapito magumu ya namna hiyo na majaribu. Mwenendo wetu ni *"kuhesabu ni furaha tupu"* tukiangukia katika majaribu mbali mbali. Zingatia kwamba Yakobo anasema "tuki" angukia katika majaribu mbali mbali, si "kama" tunaangukia katika majaribu mbali mbali. Mapito magumu na majaribu huwapata watu wote duniani kote. Kwa hiyo, tunaposongwa na misongo ya mawazo na kukumbwa na masumbufu mengi, tusifiki kwamba Mungu ametuacha au kwamba tunaadhibiwa kwa sababu ya dhambi au kuwaza kwamba kama tungekuwa na imani zaidi tusingepatwa na magumu hayo. Badala yake, Yesu mwenyewe alikabiliwa na kila aina ya magumu na alisema, *"Ulimwenguni mnayo dhiki"* (**Yohana 16:33**). Vivyo hivyo, twapaswa kuelewa kwamba matatizo tunayoyapata si ya kipekee lakini hayo yenyewe ni *ushahidi halisi kwamba Mungu anatenda kazi ndani ya maisha yetu kufunua na kuisafisha imani yetu kwa moto ili kutubadilisha katika sura ya Yesu Kristo!*

   Sababu ya kukabili majaribu yetu kwa furaha inapatikana katika **mst.3-4**: "tunajua" kwamba Mungu ni mkuu na anatumia majaribu "kuijaribu imani yetu" ili kujenga *saburi* ambayo italeta matokeo ya sisi kuwa *"wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na cho chote."*[5] Neno lililotafsiriwa kuwa

[5] Twaweza kufarijika tunapopita katika mateso kwa dhahiri kwa sababu ya imani yetu, kama mitume katika **Matendo 5:40-**

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

"saburi" ni *hupomonē* ambalo "ni tabia ya mwenendo ambao hauruhusu mtu kukubali kushindwa na hali ya mambo au kushindwa na majaribu" (Zodhiates 1993: *"hupomonē,"* 1425). Neno lililotafsiriwa "kamilifu" ni *teleois* ambalo humaanisha kuwa ni "mtu ambaye amefikia ukomavu wa kimaadili, lengo ambalo ndilo alilokusudiwa kulifikia, ambalo ni, kuwa mtu ambaye anamtii Kristo" (Zodhiates 1993: *"teleois,"* 1372). Kwa maneno mengine, Mungu hutumia majaribu katika maisha yetu ili kutufanya tuwe watu wakomavu kimaadili wenye mwenendo imara ambao, kama Yesu mwenyewe, anaweza kukabili hali mbaya za maisha akiwa na roho ya furaha, tumaini, amani, na upendo. Kwa hiyo, mtu anaweza kuiangalia mistari hii kama njia muhimu ambayo kwayo Mungu hujenga "tunda la Roho" ndani yetu (angalia **Gal 5:22-23**). Kile ambacho Yakobo anakisema kinafanana na kile ambacho Paulo anasema katika **Rum 5:3-5** na kile anachosema Petro katika **1 Pet 1:6-9**.

3. <u>Swala la majaribu na vishawishi linazungumziwa katika kitabu chote.</u> Kitabu chote kinaweza kuonekana kama kazi ya mistari mitatu ya hapo juu. Hivyo, "hekima" ya **Yak 1:5** inahusiana hapo nyuma na "kufahamu" kwa **mst.3**. Mjadala kuhusu matajiri na maskini katika **mst.9-11** huonekana katika muktadha wa kuyakabili majaribu (umaskini ama utajiri yote ni majaribu au vishawishi ambavyo hupima imani ya mtu). **Yak 1:12-15** tena huibua bayana swala la majaribu na vishawishi kwa mara nyingine. Zaidi ya hapo, kama ilivyoonyeshwa katika utangulizi, sehemu ya kitabu iliyobaki hurudia na kufafanua swala lililoibuliwa katika **Yakobo 1**. Kitabu chote, kwa asili, kinahusu vile imani halisi ilivyo—na imani halisi hatima yake huonekana pale tu itakapokuwa imepimwa na majaribu na vishawishi.

**<u>1:5-8</u>—**[5] ***Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.*** [6] ***Ila aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku.*** [7] ***Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana.*** [8] ***Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote.***

Maneno "lakini" na "akipungukiwa" huunganisha mistari hii na **mst.2-4**. Inatuonyesha sisi kwamba ufunguo wa kufanikiwa katika saburi na kushinda majaribu na vishawishi ni *hekima*. Hekima ni ufunguo kwa sababu inakwenda juu ya maarifa: hekima huunganisha maarifa na namna ya kuyatumia. Hekima ni "kujua" (**mst.3**) ya kwamba Mungu yuko nyuma ya majaribu na anayatumia kwa kusudi jema na pia hutuonyesha *jinsi ya kuyakabili* majaribu na vishawishi. Inatupa mtazamo ulio wazi wa hali yetu kwa *mtazamo wa Mungu*, sio kwa mtazamo wetu ambao unaweza kupotoshwa na kugeuzwa kwa sababu ya maumivu na mateso. Kwa kutumia hekima tunatambua kwamba taabu yetu, bila kujali chanzo chake, ni fursa ya Mungu kuleta kusudi lake katika maisha yetu.

Mistari hii pia inatujulisha ya kwamba anayetuwezesha kukabili majaribu na vishawishi vyetu kwa mafanikio ni Mungu mwenyewe. Yeye ndiye "*awapaye wote kwa ukarimu"* (**mst.5**). Zaidi ya hapo, tunajua kwamba Mungu ndiye atupaye mahitaji yetu kwa ajili ya hekima kwa sababu yeye ndiye chanzo cha hekima (**Ayu 12:13; Mith 2:6; Isa 11:2; Luka 21:15; 1 Kor 2:13; Efe 1:16-19; Kol 2:2-3; 3:16; Yak 3:17**).

Ile "imani" ambayo kwayo tunapaswa kuomba (**mst.6**) si "imani itokanayo na nguvu ya mombi" au "imani itokanayo na nguvu ya imani." Imani si "nguvu" fulani ya kimazingaombwe. Bali, imani ya kibiblia kimsingi ni kumtegemea Mungu na kujikabidhi maisha yako kwa utii kwa Mungu kupitia Kristo kwa kuangalia alichokisema. Hivyo, katika AK, kifungu kimoja cha maneno kuhusu imani au kuamini huelezea dhana ya "heshima kwa au imani kwa mtu au kitu [ikimaanisha, Mungu]"; kifungu kingine cha maneno ya Kiebrania ambacho huelezea dhana hiyo hiyo "kinaonekana sana katika Biblia ya Kiebrania lakini kwa kawaida hutafsiriwa 'kutegemea' badala ya 'kuwa na imani/amini'" Hivyo, "Utashi wa Ibrahimu kumtegemea Mungu . . . humfanya yeye kuwa mfano wa msingi wa dhana ya kibiblia imani. Utashi wake wa kumwamini na kumtii Mungu ni utimilifu wa agano ambalo Mungu alilifanya na yeye." (Schowalter 1993: 222) Dhana ya AJ ya imani ni sawa na hiyo, tofauti ya msingi ni kwamba kiini cha imani ya mtu huwa ni Yesu Kristo. Hivyo, lugha ya imani inatumika "katika kuitambua mamlaka ya kiungu ya Yesu kimatendo na pia katika kuwa na mwitiko sahihi kwa injili ambayo amekuja kuihubiri" (France 1992: 223). Hili hutuambia kwamba kuna msimamo na kutobadilika kuhusiana na imani halisi ambayo haitegemei wala kubadilika kutokana na hali za mabadiliko ya nje bali ina msingi katika uhusiano ambao uko hai kwa Bwana.

---

**41**. Hata hivyo, kiukweli majaribu hufanyika kuwa "kipimo cha imani yetu" tunapopimwa na kuonekana tuna saratani, tumeumizwa vibaya katika ajali, au mateso mengine yakitupiga *kwa sababu ambayo hatuwezi kuitambua kwa namna yoyote*. Katika hali za namna hiyo, imani yetu inawekwa katika kupimwa kwa sababu tunaweza tu *"kutembea kwa imnai si kwa kuona"* (**2 Kor 5:7**).

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Huu msimamo na kutokubadilika kwa imani huonyeshwa—"shaka." Yakobo anamzungumzia mwenye shaka ni *"kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku … mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote"* (**mst.6, 8**). Kwa maneno mengine, mtu kama huyu yuko juu siku moja na chini siku inayofuata, akiendeshwa na matukio ya nje sio uhakika wa imani wa ndani. Douglas Moo anaeleza, "Kile anachokikosoa Yakobo katika mistari hii si kuhusu mtu yule ambaye anakuwa na shaka kwa vipindi fulani kuhusiana na imani yake, au hujikuta akitenda dhambi hapa na pale—ni wachache kwa hakika ambao maombi yao yangejibiwa ikiwa hivyo ndivyo inavyomaanisha! Badala yake, Yakobo anakemea yule mtu ambaye kimsingi si mwenye nia ya kweli katika kutafuta vitu kama hekima kutoka kwa Mungu; ni mtu yule ambaye hutafuta kuwatumikia mabwana wawili tofauti kwa wakati mmoja (angalia Math. 6:24; Yakobo 4:4)." (Moo 1989: 1154) Ronald Ward anaiweka hivi, "*kuona shaka* si kutokuamini au ile falsafa ya kushuku. Sifa yake ni mpasuko wa ndani. Mwenye shaka anakubali na kukataa; anaishikilia ahadi—na ana hakika haitatimizwa." (Ward 1970: 1224) Ni majaribu na vishawishi ndivyo ambavyo kwa pamoja huiweka wazi hali ya imani yetu na hiyo husaidia kukua kwa imani yetu na tegemeo letu kwa Bwana anapotenda kazi ndani na kupitia sisi katika majaribu na vishawishi.

**<u>1:9-11</u>—*[9] Lakini ndugu asiye na cheo na afurahi kwa kuwa ametukuzwa; [10] bali tajiri kwa kuwa ameshushwa; kwa maana kama ua la majani atatoweka. [11] Maana jua huchomoza kwa hari, huyakausha majani; ua lake huanguka, uzuri wa umbo lake hupotea; vivyo hivyo tajiri atanyauka katika njia zake.***

Mjadala huu wa matajiri na maskini pia unaibuka katika muktadha wa saburi wakati wa majaribu—hapa ni kuhusiana na watu walio katika hali tofauti za kiuchumi. Umasikini wenyewe tu waweza kuwa jaribu gumu. Hata hivyo kuwa tajiri pia ni jaribu; utajiri huleta pamoja nao majaribu makubwa ya kuugawa uaminifu wetu. Mawazo yanayoelezwa hapa ni sawa na yale ya **Mith 30:8-9**: *"Usinipe umaskini wala utajiri; Unilishe chakula kilicho kadiri yangu. Nisije nikashiba nikakukana, Nikasema, 'Bwana ni nani?' Wala nisiwe maskini sana nikaiba, Na kulitaja bure jina la Mungu wangu."* Ufunguo hapa, kama inavyoonekana katika **Yak 1:9-11**, ni kufokasi kwa Bwana na hali yako ya milele, sio kuangalia hali ya kiuchumi ya nje. Yakobo anasema kimsingi kile ambacho Kristo alikisema katika **Math 6:19-21**: *"[19]Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; [20] bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; [21] kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako."* Douglas Moo anaiweka hivi: "Yakobo, hapo, anawahimiza Wakristo walio maskini na walio matajiri kukumbuka kwamba msingi mmoja mkubwa wa imani yao ni utambulisho wao na Yesu Kristo. . . . Wakristo hao wote walio katika makundi mawili, kwa maneno mengine, lazima wayaangalie maisha yao kutoka katika mtazamo wa mbinguni, sio wa duniani." (Moo 1985: 69)

**<u>1:12-15</u>—*[12] Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaandalia wampendao. [13] Mtu ajaribiwapo, "asiseme, Ninajaribiwa na Mungu," maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu. [14] Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa zake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. [15] Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.***

Katika mistari hii Yakobo kwa uwazi kabisa anarudi katika dhamira ya **mst.2-4**. Hata hivyo, **mst.12** unakwenda mbele zaidi ya **mst.4** kuhusiana na thawabu ya kuwa mwaminifu unapopita katika majaribu kwa kuingiza elementi ya thawabu ya wakati ujao—ile *"taji ya uzima"*—ya kwamba wale wanaovumilia wataipokea. Hiyo inabaki hivyo pamoja na mkazo wa Yakobo katika **mst.9-11** ya kwamba watu wanahitaji kuwa na fokasi katika hali yao ya milele, na sio katika hali yao ya muda ya kiuchumi.

**Yak 1:13-15** ni uchanganuzi muhimu na mkubwa wa asili ya majaribu na dhambi. Mistari hii huweka wazi dondoo muhimu kadhaa:

1. <u>Katika **mst.12**, neno lililotafsiriwa kama "jaribu" (*peirasmos*) ni neno lile lile lililotumika katika **mst.2**; katika **mst.13-14**, maneno yaliyotafsiriwa kama "ajaribiwapo" na "jaribu" (*peirazō*) ni muundo wa tendo la neno lile lile la Kiyunani.</u> Muktadha unaonyesha ya kuwa tafsiri sahihi katika **mst.12** ni "jaribu" na katika **mst.13-14** tafsiri sahihi ni "kushawishiwa." Hata hivyo, ingawaje maneno yanayofanana yametumika, katika **mst.2** na **12** hali za nje ndizo zinazozungumziwa, lakini katika **mst.13-14** matamanio ya ndani ndiyo yanayozungumziwa.
2. <u>Mistari inaonyesha kwamba ile asili ya dhambi—na ile asili ya kweli ya majaribu yenyewe—iko *ndani yetu.*</u> Mazingira yetu ya nje, watu wengine, na shetani mwenyewe wakati wote hutupa sisi fursa ya kuonyesha uaminifu au kutenda dhambi. Lakini hata kama mazingira yawe kinyume chetu kwa

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

nguvu kubwa kiasi gani pamoja na watu wenye ushawishi mkubwa wakiungana na shetani hawawezi kutuweka sisi hatarini *ispokuwa na mpaka tumeyakubali mapendekezo ya shetani kuwa ya kwetu*. Majaribu yako ndani sio nje. Watu wawili wanaweza kukabiliwa na hali zinazofanana za nje, lakini mmoja akatenda dhambi na mwingi asitende. Kwa mfano, mtu maskini ambaye ana uhitaji mkubwa anapoona pochi ambayo haina ulinzi; kwamba ataamua kuiiba au la itategemeana na ukweli kwamba yeye "anavutwa na kudanganywa na tamaa zake mwenyewe" au la. Mfanya biashara, mwenye mke, akiwa peke yake, mbali kabisa na nyumbani anakutana na mwanamke mrembo ambaye anataka alale naye; kwamba atalala naye au atakuwa mwaminifu kwa mke wake itategemea ule ukweli kwamba yeye "anavutwa na kudanganywa na tamaa zake mwenyewe" au la. Yakobo anatujulisha kwamba ule usemi unaotambulika sana, "ni shetani ndiye kanifanya nitende dhambi," sio kweli. Shetani hawezi kutufanya tufanye kitu ambacho hatupendi kufanya. Sisi wenyewe tunawajibika kwa cho chote tunachokifanya, na Mungu kwa halali anaweza kutuwajibisha kwa matendo yetu. Kwa asili, Yakobo anasema kile ambacho Yesu alisema katika **Math 15:19**, ya kwamba *"moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano."*

3. Neno lililotafsiriwa kama "tamaa mbaya" katika **mst.14-15** ni *epithumia.* Ingawaje neno hili "tamaa mbaya" mara nyingi lina maana ya kutaka ngono, hiyo siyo maana yake ya msingi hapa. *Epithumia* kimsingi ina maana "kutamani kwa nguvu, tamanio kubwa, hamu ya kutaka"; hasa hasa linapotumika katika dhana mbaya humaanisha "tamaa isiyo na utaratibu na isiyo na mpaka, hamu, tamaa mbaya" (Zodhiates 1993: *"epithumia,"* 627). Kimsingi, mistali hii inatuambia sisi wakati wote na tunafanya yale tu *yale tunayoyatamani sana*. Kwa mfano, ikiwa mwajiri wetu anatuambia kwamba inabidi tuseme uongo kuhusu jambo fulani la sivyo tutapoteza kazi, kama tutasema uongo haitakuwa kwa sababu "tumelazimishwa kinyume cha utashi wetu" lakini ni kwa sababu tulikuwa twataka kutunza kazi yetu badala ya kuwa mtu mwenye maadili na kusema kweli. Ikiwa katika yale mauaji ya kimbari kule Rwanda, tungeambiwa tumuue mtu fulani na tusipofanya hivyo basi sisi wenyewe ndio tungeuawa, kama tukimuua yule mtu, itakuwa ni kwa sababu ya tunataka kuishi zaidi ya kuitii amri ya Mungu, *"Usiue"* (**Kut 20:13**). Wakati fursa (hali zetu) zinapokutana na tamaa, ndipo mimba hutokea. Mimba ya dhambi wakati wote huleta mauti.

Sifa hizi zimekuwa hivyo tangu wakati wa wanadamu wa kwanza (Adamu na Hawa) ambao walitenda dhambi ya kwanza (kula tunda walilokatazwa wasilile): Wakati Hawa *"alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza kwa macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala"* (**Mwz 3:6**). Kwa maneno mengine, walitamani kula lile tunda kwa ajili ya manufaa ambayo walidhani wangeyapata zaidi ya vile walivyotamani na kumtegemea na kumtii Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo wakati wote, tunatenda dhambi kwa sababu tunataka kufanya hivyo.

**1:16-18:** ***[16] Ndugu zangu wapenzi, msidanganyike. [17] Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka. [18] Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake.***

Mstari **16** unahitajika katika **mst.14-15** na pia katika **mst.17-18**. Hiyo mistari minne huonyesha tofauti iliyo imara:

| mst.14-15 | mst.17-18 |
|---|---|
| **Jaribu** = akivutwa na kudanganywa na **tamaa zake mwenyewe** | **Kila kutoa kuliko kwema na kila kitolewacho kilicho kamili** hutoka juu kwa **Baba** |
| **Tamaa—hubeba mimba na kuzaa dhambi** | **Yeye—alituzaa** kwa **mapenzi yake na kwa Neno la kweli** |
| **Dhambi** huleta **mauti** | **Sisi** tuwe **limbuko** miongoni mwa viumbe vyake |

Sifa za "limbuko" (**mst.18**) ni pamoja na zifuatazo:

- Mazao ya kwanza (**Kut 23:19**)
- Yasiwe na chachu (**Law 2:11-12, 14**), yaliyo bora (**Hes 18:12**), kamilifu bila hitilafu (**Hes 28:31**)
- Yenye kumheshimu Bwana (**Mith 3:9**)

Kama "mazao ya kwanza," maisha yetu yanaziakisi sifa hizo hapo nyuma.

- Mazao ya kwanza yaliwatunza makuhani (**Hes 18:8-12; Ezek 44:30**); sasa sisi, kanisa, tu *"ukuhani mtakatifu"* (**1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6**), inamaanisha, tunapaswa kutunzana.
- Fungu la makuhani lilikuwa ni kwa ajili yao ili "*hao wajibidiishe katika torati ya Bwana"* (**2 Nyak 31:4-5**); sasa sisi tunapaswa *"kukaa [kuendelea] katika Neno langu"* (**Yohana 8:31**) na kuwa *"watendaji*

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

*wa Neno"* (**Yak 1:22**).

- Mazao ya kwanza huonyesha kwamba Mungu atawakubali Israeli (**Law 23:10-11**); sasa sisi, kanisa, ndio "tohara ya kweli" (**Fil 3:3**), wana wa Ibrahimu wa kweli (**Gal 3:29**), hekalu la kweli (**1 Kor 3:9, 16-17; 2 Kor 6:16-7:1; Efe 2:21; 1 Pet 2:5; Ufu 3:12**; **13:6**), "wenyeji wa Israeli" wa kweli (**Efe 2:12, 19**), Israeli wa kweli wa Mungu (**Gal 6:16**).

Mstari **18**, kama **mst.16**, ni mstari mpito. Unahitimisha kile ambacho amekuwa akikisema Yakobo hadi kufikia hapo, kuanzia **mst.2**. Fokasi yetu inapaswa kuwa kwa Mungu; anatupa sisi hekima ya kuweza kuyakabili majaribu kwa mafanikio (**mst.5**); yeye hatujaribu sisi ili tutende dhambi (**mst.13**) lakini, badala yake, anatupa vitu vyote vilivyo vyema (**mst.17**). Sababu ya haya yote ni kwamba yeye *"alituzaa sisi kwa neno la kweli"* (**mst.18**), inamaanisha, ametufanya upya, na kutupa maisha mapya, na kutuokoa (**Yohana 1:12-13; Efe 2:8-9**). Lakini ametuokoa kwa kusudi, ili *"tuwe kama limbuko la viumbe vyake"* (**mst.18**). hiyo inaonyesha kuwa ndiyo dhamira ya sura ya 1 na, hakika, na hata ya kitabu chote.

**<u>1:19-20:</u>** ***[19] Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; [20] kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu.***

Mara kwa mara twaingia hatiani kwa maneno yetu tuyasemayo kwa haraka haraka, bila ya kufikiri wala kuwa na kiasi—iwe ni kusengenya au hasira. Zaidi ya hayo, tu wenye haraka kujihesabia haki ya kukasirika, inamaanisha kwamba, tukifikiri kwamba tumekosewa hivyo tulikuwa na haki ya kukasirika, na ya kwamba Mungu yuko upande wetu. Mienendo ya namna hii hupelekea sisi "*kurudisha ovu kwa ovu au tusi kwa tusi"* (**1 Pet 3:9**). Hiyo ni kinyume cha maisha ya neema ambayo twapaswa kuyaishi. Katika maisha yenye neema, haturudishi ovu kwa ovu au tusi kwa tusi bali tuna "*toa Baraka badala yake"* (**1 Pet 3:9**).

Neno la Kiyunani kwa neno "hasira" ni *orgē* ambalo humaanisha "hasira kama hali ya namna akili yako ilivyo" kinyume chake neno *thumos* ambalo humaanisha "ghadhabu kama itokayo kwa nia ya kutaka kulipiza kisasi" (Zodhiates 1993: *"orgē,"* 1055). Yakobo anarudia maneno ya Yesu ambaye alisema kwamba uovu na kile kinachomtia mtu unajisi kinatoka ndani yake huyo mtu (**Math 15:15-20; Marko 7:14-23**). Kwa hiyo, ni lazima kuilinda mioyo yetu, fahamu na hisia. Kwa kuwa *"wepesi kusiki, bali si wepesi kusema; wala kukasirika,"* tutaepuka dhambi ya kuwa wenye kuhukumu na hivyo sisi wenyewe tutaepuka kuhukumiwa au kuadhibiwa (angalia **Math 7:1-2**).

**<u>1:21-27:</u>** ***[21] Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu. [22]lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. [23]Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. [24]Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. [25]Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake. [26]Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai. [27] Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.***

Hii sehamu ndefu ya mwisho ya sura ya 1 hukupa picha ya ujumla ya kitabu chote kilichobaki; sehemu iliyobaki ya kitabu hushughulika na matumizi bayana ya kanununi zilizojadiliwa hapa. Ufunguo wa jinsi ya kuishi maisha ya uaminifu katika Neno la Mungu. Kwa hiyo, ingawaje *"hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu"* (**mst.20**), neno la Mungu, linapoingia ndani ya nafsi ya mtu, humpatia haki ya Mungu—hilo pekee *"linaweza kuziokoa roho zenu"* (**mst.21**). Hata hivyo, neno halipaswi kusomwa au kukaririwa tu; badala yake, inabidi liwekwe katika matendo. Kwa hiyo, **mst.22** unatuambia *"iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu."*

Mstari **21** unatukumbusha kwamba tumezungukwa na uchafu wa kimaadili. Ikiwa tutairuhusu hali hiyo ipate nafasi ndani yetu itatupeleka katika uovu. Neno la Kiyunani lililotafsiriwa "uchafu" hapa ni *kakias* ambalo humaanisha "uchafu kama tabia ovu ya ufahamu . . . uovu katika maana ya kimaadili humaanisha uovu wa moyo, maisha na mwenendo" (Zodhiates 1993: *"kakia,"* 807). Kama alivyofanya katika **mst.19-20**, Yakobo anakwenda katika moyo wa jambo hilo: ndani mwetu, sisi hasa. Tunaweza tu "kupokea neno" kwa *unyenyekevu.* Hivyo huturudisha katika **mst.19-20** kwa sababu unyenyekevu ni kinyume cha ubinafsi na hasira ya mistari hiyo. Unyenyekevu ni kutambua kwamba lile neno tunalolipokea linalookoa nafsi zetu linatolewa kwetu kwa neema ya Mungu hasa, si kwa sababu ya chochote kile tulichofanya. Hatulipati kwa kulitendea kazi; linatolewa kwetu licha ya—kwa hakika, kwa sababu ya—dhambi zetu, kushindwa, na kutokustahili. Tunapoelewa hayo

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

sawasawa, hatuwezi kukosa kuwa na mwelekeo sahihi wa hali ya moyo na ufahamu ambao Yakobo anauzungumzia.

Mstari **22-25** huweka kanuni inayotuongoza: *"iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu"* (**mst.22**). neno ni kioo cha maisha yetu (**mst.23-25**). Vile vile neno ndicho kipimo ambacho kwacho tunaamua yale ambayo tunapaswa kufanya katika maisha yetu. Neno linatuonyesha namna tunavyopaswa kuishi. Lakini neno ni zaidi ya hapo. Katika **mst.25** neno linaitwa *"sheria iliyo kamilifu iliyo ya uhuru."* Hii ni kwa sababu neno hutuweka huru kutoka katika uwongo. Kama Yesu alivyosema, *"Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, na hiyo kweli itawaweka huru"* (**Yohana 8:31-32**). Neno pia hutuweka huru kutoka katika vifungo vya nguvu na matokeo mabaya ya dhambi; kama **mst.21** umesema, neno lililo ndani yetu huokoa nafsi zetu. Kwa hiyo, neno, linalotenda kazi, ni ile injili ambayo imetuweka huru kutoka katika vifungo na adhabu ya dhambi na ya kwamba sasa sisi si watumwa tena wa dhambi (**Rum 6:6-7**). Si kwamba neno linatuweka huru tu *kutoka* uwongo na dhambi, pia linatuweka huru na kutuwezesha kumjua Mungu, kumwabudu Mungu, kufikiri sawa sawa, na kuishi sawa sawa. Kwa hiyo, **mst.25** unatoa ahadi ya Baraka kwa wale watendaji wa neno. Kwa kufanya hivyo, Yakobo anarudia yale ambayo Yesu alisema katika **Luka 11:28** (ESV): *"Afadhali, heri walisikiao neno la Mungu na kulishika!"* Hata hivyo, zile Baraka na faida za neno zitakuwa zetu endapo "tutaangalia kwa makini" hilo neno. Kwa maneno mengine, tunajifunza neno, tunalifanyia kazi, tunakariri neno, tunatekeleza maagizo yake kwa vitendo kiasi kwamba lile neno linakuwa "limezama" katika vilindi vya utu wetu. Kwa kifupi, tunakuwa watu wa neno.

Mistari **26-27** inahitimisha kile ambacho Yakobo amekuwa akikisema kwa kutoa tafsiri ya kile ambacho Mungu anakitambua kuwa ni "dini iliyo safi." Neno lililotafsiriwa kama "dini" katika mistari hii ni *thrēskeia* ambalo humaanisha "taratibu za kidini au ibada" (Zodhiates 1993: *"thrēskeia,"* 742) au "udhihirisho wa kujitoa kwa nafsi zilizo juu ya uwezo wa mwanadamu, hasa, kama inavyojidhihirisha katika kaida za imani potofu" (Danker 2000: *"thrēskeia,"* 459). Kwa maneno mengine, inazungumzia taratibu za matendo ya kidini ambayo yana maana mbele za Mungu. Watu wanafanya mambo mengi ya mapokeo ya kidini: wengine wana piga magoti katika kuabudu (wanapiga magoti au wanagusisha goti moja sakafuni kuonyesha uchaji kwa Mungu); wengine hufanya ishara ya msalaba; wengine huinua mikono yao wanapoomba; wengine huinamisha vichwa, hufumba macho, na kukunja mikono yao. Yakobo anasema kwamba matendo halisi ya kidini ambayo Mungu anayathamini si kupiga magoti, au kuinamisha vichwa, nk. lakini ni *"kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa"* (**mst.27**).

Yakobo anaonyesha kwamba *"dini iliyo safi isiyo na taka mbele za Mungu Baba"* inahusisha mtu kamili ndani na nje. Ukijiaangalia mwenyewe *"kujilinda na dunia masipo mawaa"* kimsingi inahusiana na utu wetu wa ndani, ina maana, "usichafuliwe" na viwango, vipaumbele na mitazamo ya kidunia. Hili ni muhimu kwa sababu "jamii huakisi, kwa sehemu kubwa, imani na itikadi ambazo ziko kinyume na Ukristo, kama hazipingi kabisa Ukristo. Mwamini aishiye 'duniani' yuko katika hatari kila wakati kuchafuliwa na mawaa ya mifumo 'ikikwaruza juu yake." (Moo 1985: 87) Rai hii huturudisha kwenye **mst.21** ambapo Yakobo alituambia kuweka mbali *"uchafu wote na ubaya uzidio."* Tunafanya hayo kwa kuweka ufahamu wetu *"kwenye yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi"* (**Kol 3:2**). Tunafanya hayo kwa *"kuteka nyara kila fikra ipate kumtii Kristo"* (**2 Kor 10:5**) na kwa kufokasi kwenye *"mambo yo yote yaliyo kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema,"* vizuri sana, inastahili kusifiwa (**Fil 4:8**). Kwa kifupi, tunapaswa "*kutafuta kwanza ufalme Wake na haki yake"* (**Math 6:33**) na *"kumpenda Bwana Mungu kwa moyo wangu wote, na kwa roho yangu yote, na kwa nguvu zangu zote na kwa akili yangu yote"* (**Luka 10:27**; angalia pia **Math 22:37**), ambayo ndiyo amri ya kwanza na kubwa kuliko zote (**Math 22:38**).

Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki zao huzungumzia kuhusiana na udhihirisho wa nje wa kujitoa kwetu kwa Mungu. Hiyo ni ishara ya nje inayoonekana ya kile ambacho kiko ndani, neema ya kiroho ndani ya maisha ya mtu. Hiki ndicho kile ambacho Yesu alikiita amri ya "pili", *"mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Math 22:39**; angalia pia **Luka 10:27**). Kujali na kuhusika ambako tunapaswa kuwaonyesha wengine hakuishii tu kwa "yatima na wajane." Kwa hakika, "'yatima na wajane' katika Agano la Kale kilikuwa kipimo kinachojieleza ya kuwa hawa walikuwa ndio wale wasiojiweza duniani" (Moo 1989: 1155). Yesu aliliweka hili wazi alipokuwa akizungumza kuhusu hukumu ya kondoo na mbuzi. Alisema, *"[35] Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; [36] nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia.' [37] Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? [38] Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? [39] Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia?' [40] Na mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."* Mtume Yohana alikazi kwamba matendo yetu ya nje ya kuonyesha upendo kwa wengine ni kithibitisho, kipimo, cha kama tunayo imani halisi iokoayo au

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

la. Katika **1 Yohana 4:20** anasema, *"Mtu akisema, 'Nampenda Mungu,' naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."* Kwa kifupi, "dini iliyo safi' ya 'Mkristo mkamilifu' (v. 4) huchanganya usafi wa moyo na usafi wa matendo" (Moo 1985: 87).

Sura ya kwanza ya Yakobo imeshughulika na maswali yaliyo muhim zaidi ya maisha yetu na imani yetu: kuanzia majaribu na jinsi ya kuyashinda, hadi dhambi na asili yake, mpaka namna tunavyotakiwa kuishi, na kuishia na maana ya dini iliyo safi mbele za Mungu. Ameendelea hadi katika moyo wa swala lenyewe. Maelezo yake kuhusu asili ya dini iliyo safi katika **mst.27** kwa kweli inatupeleka kule ambako imani yetu inapaswa kutufanya tuwe: tunapochota hekima ya Mungu na kuiishi imani yetu, tutaidhihirisha tabia ya Mungu mwenyewe ambaye ni *"Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane"* (**Zab 68:5**) na ambaye, katika hali ya utu wa Yesu Kristo, *"alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi"* (**Ebr 4:15**), ina maana, *"hakuchafuliwa na dunia."* Ni kwa namna gani inawezekana kuishi maisha ya jinsi hiyo katika mazingira bayana ndilo somo linaloendelea katika sehemu yote ya kitabu iliyobaki. Kwa hayo sasa ndiyo tunaendelea.

## MASWALI YA KUJADILI

1. Kwa nini Yakobo analiita kanisa (ambalo analiandikia waraka huu) "kabila kumi waliotawanyika" katika Yak 1:1?

2. "Majaribu" ni nini, na kwa nini na kwa namna gani "tuhesabu ni furaha tupu" tunapokutana na majaribu mbalimbali (angalia Yak 1:2-4)?

3. "Hekima" tunayopaswa kumuomba Mungu ni ipi (Yak 1:5)? Ni kwa nini ni ya muhimu sana?

4. Yak 1:6 inasema tumuombe Mungu kwa "imani." Ielezee asili na sifa za imani.

5. Ni dokezo gani muhimu ambalo Yakobo analitoa katika Yak. 1:9-11 katika mjadala wake kuhusu matajiri an maskini?

6. Katika Yak 1:12-15 Yakobo anazungumzia kuhusu majaribu na vishawishi.
   - Kuna tofauti gani kati ya majaribu na vishawishi?
   - Katika Yak 1:14-15 Yakobo anatumia neno "tamaa." "Tamaa" ni nini kama Yakobo anavyolitumia?
   - Kutokana na mistari hii, chanzo cha dhambi ni nini?
   - Ni kwa namna gani Mungu anatumia majaribu yetu na vishawishi tunavyokutana navyo kutufanya tukomae na tuwe kama Kristo?

7. Ni zipi ni sifa za "malimbuko" (angalia Yak 1:16-18), na maisha yetu yanapaswa kuonekanaje kwa kuwa tunapaswa kuwa "aina ya wazaliwa wa kwanza miongoni mwa viumbe Wake"?

8. Yak 1:19-21 inaorodhesha vitu muhimu kadhaa ambavyo hupaswa kuwa ni sifa ya maisha ya Mkristo. Ni vitu gani hivyo? Kanisa litawezaje kuwasaidia watu wake kukua katika maeneo haya?

9. Yak 1:22-25 hujadili kanuni ya msingi ya kuwa watendaji wa Neno, sio tu wasikilizaji wa Neno. Kwa kupitia huduma zake za kuhubiri na kufundisha, kanisa linaweza kuwasaidia watu wake kujifunza Neno. Lakini ni nini kinaweza na kinapaswa kufanyika ili kanisa liwasaidie watu wake kwenda mbele zaidi ya kujifunza Neno na kuwa "watendaji" wa Neno?

10. Katika Yak 1:26-27, Yakobo anatuambia "dini iliyo safi, isiyo na taka mbele Mungu Baba" ni ipi (m.y., "jadi au sherehe za kidini " ambazo Mungu anazithamini). Je Mungu anathamini jadi na sherehe zipi za kidini? Ni nini tunahitajika kufanya katika makanisa yetu kuweka mkazo na kufanya yale ambayo Mungu anayathamini?

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

**III. <u>Yak 2:1-13—Dhambi ya upendeleo</u>—*Ndugu zangu, imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, msiwe nayo kwa kuwapendelea watu. [2] Maana akiingia katika sinagogi lenu mtu mwenye pete ya dhahabu na mavazi mazuri; kisha akiingia na maskini, mwenye mavazi mabovu; [3]nanyi mkamstahi yule aliyevaa mavazi mazuri, na kumwambia, "Keti wewe hapa mahali pazuri;" na kumwambia yule maskini, "Simama wewe pale, au keti miguuni pangu," [4]je! Hamkufanya hitilafu mioyoni mwenu, mkawa waamuzi wenye mawazo mabovu? [5] Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni, Je! Mungu hakuwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao? [6] Bali ninyi mmewavunjia heshima maskini. Je! Matajiri hawawaonei ninyi na kuwavuta mbele ya viti vya hukumu? [7] hawalitukani jina lile zuri mliloitwa?***

***[8] Lakini mkiitimiza ile sheria ya kifalme kama ilivyoandikwa, "MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO," mwatenda vema. [9] Bali mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji. [10] Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. [11] Kwa maana yeye aliyesema, "USIZINI," pia alisema, "USIUE." Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria. [12]Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru. [13] Maana hukumu haina huruma kwake yeye asiyeona huruma. Huruma hujitukuza juu ya hukumu.***

Neno katika **mst.1** lililotafsiriwa *"kwa kuwapendelea watu"* ni neno la Kiyunani (*prosōpolēpsia*) ambalo hasa humaanisha "kuupokea uso," ina maana, kuonyesha upendeleo au kubagua (angalia Moo 1989: 1155; Zodhiates 1993: *prosōpolēpsia,* 1239). Neno liko katika wingi (inamaanisha, "matendo ya kubagua"), ambayo huonyesha kwamba, ingawaje Yakobo anatumia mfano wa upendeleo alionyeshwa mtu tajiri, aliyevaa vizuri dhidi ya maskini, aliyevaa vibaya (**mst.2-6**), *kanuni* ambayo Yakobo anaijadili katika sehemu hii inaweza kutumika katika "namna anavyotendewa mtu ye yote kwa kuzingatia muonekano wake wa nje—iwe ni mbari, utaifa, utajiri au namna ya kuvaa kwake" (Moo 1989: 1155).

1. <u>Sehemu hii inatupa theolojia pana inayotuonyesha ni kwa nini kuwapendelea watu ni dhambi kubwa:</u>

- **<u>mst.1—</u>**<u>Yesu ni Bwana wetu wa utukufu.</u> Tukiwapa baadhi ya watu ule utukufu, kama yule mtu tajiri katika mfano wa Yakobo, basi tunatenda "kana kwamba Yesu hana huo utukufu; kuingia kwa tajiri kunasherehekewa kama vile ni Bwana Yesu mwenyewe kaingia" (Ward 1970: 1227). Kuonyesha upendeleo kwa watu fulani kwa sababu ya daraja lao "haikubaliani na imani ndani ya Yeye ambaye amekuja kuvunja mipaka ya utaifa, mbari, daraja, jinsia na dini" (Moo 1985: 88; angalia **Efe 2:11-22**). Kwa maneno mengine, tunapowapa upendeleo watu wa daraja fulani kwa gharama ya watu wa madaraja mengine, kwa kweli tutakuwa tunamshusha Yesu kutoka katika nafasi aliyonayo ya ushindi dhidi ya wote, ambayo Yeye peke yake ametunukiwa kuwa nayo. Hili ni swala nyeti sana.

  Zaidi ya hayo, Mungu ndiye muumbaji wa vyote kwa hakika. Mungu hakuwaumba tu wanadamu wawili wa kwanza (Adamu na Hawa) na kisha akatuacha peke yetu. Badala yake, Mungu anamfanya *kila mtu mmoja* (**Kut 4:11; Ayu 10:8; 31:15; Zab 100:3; 119:73; 139:13-16; Isa 44:24; Yer 1:4-5; 27:5**). Kwa sababu Mungu alituumba, sisi ni wake (**Kum 10:14; Ps 24:1; 50:10-12; 95:6-7; 100:3; Isa 17:7; 29:19; 45:9; 64:8; Yer 18:1-10; Rum 9:20**). Pamoja na hayo, wanadamu wote wameumbwa kwa "mfano wa Mungu" (**Mwz 1:26-27; 5:1, 3; 9:6; Jas 3:9**). Tukiwa na haya yote, **Rum 2:11** inasema, *"Hakuna upendeleo kwa Mungu"* (angalia pia **Law 19:15; Kum 10:17**). Mstari huo unatumia neno lile lile la Kiyunani (*prosōpolēpsia*) ambalo Yakobo analitumia katika **mst. 1**. Sasa ndani ya Kristo, **Gal 3:28** inasema, *"Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wa huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu."* Maana ya hili ni kwamba, tunapoonyesha upendeleo kwa watu fulani, tunatenda kinyume na asili hasa ya tabia ya Mungu na Kristo!
- **<u>mst.4—</u>**<u>Tunapoonyesha upendeleo, tunakuwa mahakimu wenye matarajio maovu.</u> Katika **Yohana 7:24** Yesu alisema, *"Basi msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki."* Tunapoanza kubagua kwa misingi ya muonekano wa nje kama hali ya kiuchumi, mbari, kabila, nk., Mungu huiangalia hali hii kama mfumo wa kuhukumu ulio wa uovu, kwa sababu misingi ya maamuzi yake iko katika vigezo ambavyo havihusiki. Mbaya zaidi, hukumu zitolewazo kwa misingi ya vigezo vya muonekano wa nje, mara nyingi vimepambwa na vitu kama ulafi, wivu, chuki na nia nyingine zilizo *ovu*. Tunahitaji kukumbuka **1 Sam 16:7** (ESV): *"Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu hutazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo."* Kwa kiwango kile tunachoonyesha upendeleo kwa misingi ya hali za nje, tunawatathmini na kuwahukumu watu kinyume cha vile ambavyo Mungu anawatathmini na kuwahukumu watu hao.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Tunapofanya hayo, tunakuwa kama Petro wakati Yesu alipomwambia, *"Nenda nyuma yangu, Shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu."*

- **mst.5-6—**Tunapopendelea, hatuwaheshimu wale ambao Mungu amewaheshimu. Yesu mwenyewe alikuwa mtu maskini. Alisema, *"Heri ninyi mlio maskini, kwa sababu ufalme wa Mungu ni wenu"* (**Luka 6:20**).[6] Tunapobagua kwa kuangalia viwango vya madaraja ya watu tunatenda "kinyume na mwenendo na utendaji wa Mungu mwenyewe" (Moo 1989: 1156). Kwa kweli, tunamtemea mate Mungu usoni yeye ambaye amewabariki na kuwachagua watu kutoka *kila "taifa, na kabila, na jamaa, na lugha"* duniani (**Ufu 5:9; 7:9**). Kimsingi tunasema, "Mungu, una maamuzi mabaya kwa kuwapendelea watu kama hawa. Mimi nina maamuzi bora kuliko ya kwako, kwa sababu siwapendi watu kama hawa." Hebu fikiri kuhusu kiburi cha jinsi hiyo! Badala yake, twahitaji kukumbuka kwamba "Wakristo, hata wawe maskini wa vitu kwa kiwango gani, wote wana utajiri wa kiroho sasa hivi na wanatarajia baraka zilizo kuu zaidi wakati ule ujao. Ni kutokana na dhana hii ya manufaa iliyo ya kiroho, si ile ya vitu vya mwilini, ya kwamba Mkristo anapaswa kufanya maamuzi ya namna anavyowatazama wengine. Wawe ni waaminio au wasioamini, hawapaswi kutathminiwa na Wakristo kwa kufuata vigezo vya kidunia." (Moo 1985: 91)
- **mst.6-7—**Tunapowapendelea watu ambao ni matajiri wasiomcha Mungu na wenye nguvu *tunawaheshimu* wale wasiomheshimu Kristo. Katika siku za Yakobo, matajiri walikuwa wakiwanyonya walio maskini ingawaje Wakristo walio wengi walikuwa maskini. Kwa hiyo, inashangaza na ni kinyume na mshikamano na umoja wa kanisa "kuwatendea vibaya wale ambao wengi wao walivutwa ili kupata upendelea kwa matajiri na wenye nguvu" (Moo 1989: 1156). Hata hivyo, hali ni mbaya kuliko hiyo. Mstari **7** unasema, *"Hawalitukani jina lile zuri mliloitwa?"* wakristo wanabeba jina zuri la Kristo. Wale wanaowatenda vibaya, kuwakandamiza, au kuwatesa Wakristo (**mst.6**) kiuhalisia, wanamtenda vibaya, wana mkandamiza au kumtesa Yesu mwenyewe (angalia **Matendo 9:4-5**). Kumtendea Kristo namna hiyo na sawa na kulikufuru jina lake. Kama Donald Burdick asemavyo, "Kuonyesha upendeleo kwa wale wanaokufuru jina lile la ajabu ni hitilafu kubwa kuliko zote" (Burdick 1981: 179). Tena, hata hivyo, hali ni mbaya kuliko hiyo. Tunapowaheshimu na kuwapendelea wanaokufuru kwa sababu wao ni matajiri au wana nguvu, *tunashiriki madhara ya kukufuru kwao*. Paulo alizungumza kitu kinachofanana na hicho katika **1 Tim 5:22** aliposema, *"Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine."* Kile ambacho Yokobo na Paulo wanasema wote ni kwamba namna tunavyowatendea watu huwa na matokeo makubwa sana zaidi ya kile tunachokiona hasa. Wanasema kwamba kuonyesha upendeleo kwa mtu asiye mcha Mungu kwa sababu yeye ni tajiri huenda mbali zaidi ya pesa; kiuhalisia ni kuchukua dhamana ya kuikubali hali ya mtu huyo ya kutomcha Mungu na maisha yake ya kufuru.
- **mst.8-11—**Tunapoonyesha upendeleo kwa watu kwa misingi isiyo ya kibiblia, tunaivunja ile "Sheria ya Kifalme." "*Kumpmenda jirani yako kama nafsi yako"* inaitwa "Sheria ya Kifalme" kwa sababu imetoka kwa Mfalme mwenyewe. Ni ya "kifalme" kwa sababu "ni sheria kuu ambayo kwayo sheria nyingine zote zinazoongoza maisha ya mwanadamu katika mahusiano ziko chini yake" (Burdick 1981: 179). Kwa hakika, **Gal 5:14** inasema kwamba sheria yote imefupishwa na kutimilika katika tamko hili, *"Umpende jirani yako kama nafsi yako."* Kwa hiyo, *"kuonyesha upendeleo, [inaonyesha] unatenda dhambi na unahukumiwa na sheria kama mkosaji."*

Ukweli kwamba sheria yote inatimilika kwa kumpenda jirani yako kama unavyojipenda wewe hutupeleka kwenye dondoo ya Yakobo katika **mst.10**, *"ukiishika sheria yote, ila ukajikwaa katika neno moja, umekosa juu ya yote."* Ni kwa nini anasema hivyo? Sababu ni kwamba sheria *ni* kitu kizima—kama mnyororo hivi. Ukikata kiunganishio kimoja huhusisha kuukata mnyororo wote. Sheria ya Mungu ilitolewa na Yeye. Kwa hiyo, hata ile dhambi ndogo huhusisha ukosaji dhidi ya

[6] Mstari **5** unasema kwamba *"Mungu [aliwachagua] maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao."* Inapaswa kuingia akilini mwetu kwamba "Yakobo hasemi kwamba Mungu amewachagua maskini *wote* au maskini *peke yake*, lakini kwamba Mungu anahusika kimaalumu kwa walio maskini (Luka 6:20)" (Moo 1989: 1156). Zaidi ya hayo, "Mungu kuwachagua maskini isichukuliwe kama umasikini ni kigezo cha sifa inayowastahilisha. Sababu moja Mungu 'amewachagua walio maskini' inaweza kuonekana katika habari ya kijana mtawala aliyekuwa tajiri (Marko 10:17-27). Hapo Yesu alionyesha kwamba wale walio na utajiri inawawia vigumu sana kuingia katika ufalme wa Mungu (mst.23-25), kwa dhahiri mali zao huwa ndio kikwazo. Mungu huwabariki wale ambao kwa hiari wanagundua kwamba ni maskini wa roho (Math 5:3). Sababu ya pili kwa nini Mungu huchagua walio maskini imeelezwa wazi katika 1 Kor 1:26-29. Mungu anawachagua wale wasio na kitu au si kitu wao wenyewe 'ili asiwepo wa kujigamba mbele zake' (mst.29)." (Burdick 1981: 179)

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Mtoa sheria, kwa sababu inamaanisha kuyakataa mamlaka yake *yote* juu ya maeneo ya maisha yetu *yote*. Kama Burdick anavyoiweka, "Kuvunja sheria katika jambo lolote lile si kuvunja sheria moja tu, ni kuvnja mapenzi ya Mungu na kuwa kinyume na tabia ya Mungu. . . . Linapoangaliwa namna hii tendo la kuonyesha upendeleo liko mbali sana na hali ile ya udogo." (Ibid.: 180)

Mungu alitoa sheria yake kwa sehemu kuweka wazi hali za mioyo yetu. Anajua kwamba tunaangalia muonekano wa nje—lakini Yeye huangalia moyo. Tunapoonyesha upendeleo kiuhalisia tunaonyesha dharau tuliyonayo moyoni kwa mtu fulani—kwa sababu Yesu alisema katika **Marko 7:21**, *"Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi."* Chakushangaza, katika **Marko 7** na katika **Yakobo 2,** Wote Yesu na Yakobo huonyesha kuwa kuna uhusiano katika mawazo mabaya, kuua na uzinzi. Wote wanajua kwamba haya yote ni madhihirisho ya moyo ulioharibika na mwovu. Katika mantiki hiyo, kwa hiyo, kuonyesha upendeleo kwa mtu kwa misngi ya sifa za nje si tu "dhambi ndogo" fulani ambayo sote twaweza itenda. Badala yake ni mbaya sana kama ilivyo kuua au uzinzi.[7]

- **mst.12-13**—Kuonyesha upendeleo kutaleta matokeo ya kukosa rehema katika kutoa hukumu.

Siku zote Wakristo wanapaswa kujua kwamba itakuja siku moja ambayo tutahukumiwa (**2 Kor 5:10** [*"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"*]). Kama Yesu alivyosema, *"Lakini hakuna neno lililositirika ambalo halitafunuliwa, wala lililofichwa ambalo halitajulikana.* [3] *Basi, yo yote mliyosema gizani yatasikiwa mwangani; na mliyonena sikioni mwa mtu katika vyumba vya ndani, yatahubiriwa juu ya dari."* (angalia pia **Math 10:26; Marko 4:22; Luka 8:17**) Kwa kuongezea, Yesu alisema kwamba *"kwa viwango na vipimo unavyopima kwa wengine ndivyo na wewe utakavyopimiwa"* (**Luka 6:37**).

Ronald Ward anaonyesha kwamba kauli iliyo katika **mst.13** kwamba *"hukumu haina huruma kwake yeye asiyeona huruma"* inaweza kuonekana "isiyosamehe na chini ya viwango vya Kikristo. Lakini haimaanishi hivyo. Hukumu kama hukumu haina rehema. Mara tu inapoonyesha rehema inaacha kuwa hukumu kamili." (Ward 1970: 1228) Kwa maneno mengine, wale ambao katika maisha haya hawakuonyesha rehema watapokea kile ambacho wanachokistahili hasa: haki iliyo sawa. Kwa hivyo, hukumu inahusiana na "sheria ya kifalme" ya upendo. Namna tunavyowatendea watu katika maisha haya kitakuwa ndicho kipimo kitakachoamua namna ile hukumu yetu ya mwisho iwe, ile ya thawabu na ya adhabu, kwa sababu hiyo huonyesha hali halisi ya mioyo yetu na uhusiano wetu halisi na Yesu (**Math 6:1-4, 12, 14; 10:42; 24:45-51; 25:31-46; Marko 9:41-42; Luka 6:35; 12:33, 41-48; 14:13-14; 16:1-9; Rum 2:1-6; 1 Tim 6:18-19; 2 Tim 4:14; Ebr 6:10; 1 Pet 5:1-4**). Yesu analiweka hili hasa wazi katika sala ya Bwana na katika maelezo yake kuhusiana na hukumu ya Kondoo na Mbuzi. Kifungu kile cha Sala ya Bwana kinachosema *"utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu"* (**Math 6:12; Luka 11:4**) ni kifungu pekee cha Sala ya Bwana ambacho Yesu anaweka bayana na kukazia: *"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu."* (**Math 6:14-15;** angalia pia **Marko 11:23-26**) Vivyo hivyo, mafundisho ya Yesu yaliyo wazi kuhusiana na hukumu ya mwisho huonyesha kwamba kutengwa na Mungu milele au kuwa naye kwa baraka ya milele kutategemea jinsi ambavyo tumewatendea watu katika maisha haya kwa sababu: *"kadiri mlivyomtendea* [ina maana, mlionyesha kujali na huruma] *mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"* (**Math 25:40**), na *"kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi"* (**Math 25:45**). Kinachosababisha yule asiyeonyesha rehema asitarajie kupokea rehema siku ile ya hukumu "itakuwa ushahidi muhimu wa uhalisia wa uhusiano wetu na Mungu, kama ambavyo Yesu anavyoweka mkazo katika mfano wa mtumwa asiye na rehema (mst. 13; angalia Math. 18:21-35)" (Moo 1989: 1156). Maoni ya Stephen Travis kuhusiana na jambo hili huleta maana hasa kuhusiana na mfano wa Yakobo wa kutomheshimu mtu maskini na kuonyesha upendeleo kwa mtu aliye tajiri: "Jambo moja la kushangaza katika kifungu cha mbeleni [wale Kondoo na Mbuzi] ni kwa namna ile ambayo si 'kondoo' wala 'mbuzi' waligundua hivyo kwa fahamu zao ya kwamba, *katika kujali au kutokujali walio maskini*, kwa hakika wamekuwa wakionyesha mwitikio kwa Yesu. . . . Hakuna kinachoweza kuelezea kwa usahihi zaidi ya namna matendo ambayo Mungu anayakubali

[7] Kuonyesha upendeleo ni sawa na Yesu anavyofananisha tabia ya ndani ya mtu kuwa na hasira na kuua (**Math 5:21-22**; angalia pia **1 Yohana 3:15**) na tabia ya ndani ya tamaa mbaya na uzinzi (**Math 5:27-28**). Hasira na tamaa mbaya havihitaji kutendwa ili vilinganishwe na kuua na kuzini. Kuonyesha upendeleo ni vibaya zaidi, kwa sababu kuonyesha upendeleo, kwa tafsiri, ni *kumtendea mtu kwa kufuata* mwenendo wa ndani ulioharibika wa dhambi.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

hutiririka kiasili kutoka katika uhusuano mzuri na Mungu. Ni kile afanyacho mtu wakati akiwa hatafuti kutambulika ndicho kinachodhihirisha utu wake wa kweli." (Travis 1982: 191, mkazo kwenye nakala ya asili)

Kauli ya kuhitimisha ya Yakobo katika **mst.13**, *"huruma hujitukuza juu ya hukumu,"* yaweza kuchukuliwa kwamba inamaanisha rehema ile tunayowaonyesha wengine: "kuonyesha kwetu rehema *hutushindia juu ya* hukumu ya Mungu kwa kuwa hututetea sisi mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu" (Moo 1985: 98). Ikiwa maisha yetu yamejaa msamaha, upendo, na rehema, inaonyesha kwamba tumeiweka mioyoni mwetu Sala ya Bwana, ile "sheria ya kifalme," na ile kanuni ambayo Yesu aliitamka katika mfano wa mtumwa asiye na rehema, *"Nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe?"* (**Math 18:33**). Burdick anahitimisha, "Rehema inapaswa kuwa alama ya mtu aliyezaliwa upya. Ikiwa ipo katika maisha ya mwamini, hana sababu ya kuogopa siku ile ya hukumu. . . . uwepo wa upendo (au rehema) huonyesha kwamba Mungu amafanya kazi ya neema katika moyo wa mwamini, akimfanya awe kama Kristo. Matokeo yake ni kwamba, anaweza kuwa na ujasiri anapokuwa mbele ya hukumu." (Burdick 1981: 181)

2. <u>Madhara ya dhambi ya kuonyesha upendeleo:</u>

- <u>Madhara kwa mtu maskini.</u> Yule mtu ambaye amebaguliwa dhidi ya mwingine kuna uwezakano mkubwa atafikiri, "Ikiwa hivi ndivyo wanavyonitendea mimi, basi kwa nini mimi niwe Mkristo, au nije kwenye kanisa hili? Hawana tofauti na watu wa dunia." Ward anaonyesha kwamba, baada ya kuwa mhanga wa kubaguliwa, "Yule mtu maskini si rahisi yeye kuliamini Neno ambalo litakuwa linaahubiriwa wakati huo" (Ward 1970: 1227).
- <u>Madhara kwa mtu tajiri.</u> Ingawaje yule mtu tajiri atakuwa ameonyeshwa upendeleo, anajua kwamba anatumiwa. Je yeye si ndio atafikiri, "Nimepewa heshima hii kwa sababu mimi ni tajiri, kwa sababu wanataka pesa zangu. Hawa hawana tofauti na watu wa dunia."
- <u>Madhara kwa kanisa.</u> Yakobo alianza sura ya **2** kwa kuwaita waamini—kanisa—kama "ndugu." Waamini wote ni ndugu kaka na dada katika Kristo. Sisi sote tuko sawa mbele za macho ya Mungu (**Gal 3:28; Kol 3:11**) kwa sababu sisi sote ni sehemu ya familia moja (**Math 12:49-50; 2 Kor 6:18; Efe 2:19; 1 Tim 3:15; 5:1-2**). Kwa hakika, sisi sote tumeasiliwa katika familia ya Mungu (**Rum 8:14-17, 23; Gal 3:25-4:7**). Kwa hiyo, kuonyesha ubaguzi *miongoni mwa Wakristo* kwa misingi ya vigezo vya sifa za nje, ambazo hutazamwa na wasioamini, ni dhambi kubwa kwa sababu inapiga katika moyo wa Kristo kuhusiana na kile alichokifanya kwa kutuokoa sisi sote sawasawa, kwa kutupa sisi sote Roho Mtakatifu sawasawa, na kutuasili sisi sote katika familia yake sawasawa. Kumpendelea mtu fulani tajiri *asiye Mkristo* dhidi ya aliye maskini "ndugu katika Bwana" ni vibaya sana zaidi ya hayo mengine. Tabia ya namna hiyo huligawa kanisa. Kile ambacho Kristo amekiunganisha pamoja tusikitenganishe.
- <u>Madhara kwa wasioamini.</u> Asiyeamini anapotuona sisi tunabagua kwa misingi isiyo ya kibiblia, kwa kuangalia vigezo vya muonekano wa nje, je yeye si atafikiri, "Ikiwa Wakristo na Ukristo ndivyo hivi ulivyo, basi kwa nini niwe Mkristo? Hawana tofauti na watu wa dunia."

Kile tunachofanya katika maisha haya—hasa hasa namna tunavyowatendea watu—kina matokeo ambayo hatuwezi kuyaona. Zaidi ya hayo, kile tunachofanya kina matokeo si tu katika maisha haya bali hata katika maisha ya milele. Tunahitaji kuliweka hili katika ufahamu wetu kila wakati tunapoendelea na maisha yetu ya kila siku. Ndiyo maana Biblia inasema, *"Tukiteka nyara kila fikra ipate kumtii Kristo"* (**2 Kor 10:5**). Tunapofanya haya, tutaanza kuisha kwa kumaanisha zaidi. Tutaanza kuishi maisha yanayomfanania Kristo zaidi. Tutaanza kuwa kama Kristo Mwenyewe.

## <u>MASWALI YA KUJADILI</u>

1. Jadili "dhambi ya upendeleo" fokasi ya Yakobo ni ipi 1:1-13. Ni kwa namna gani tofauti tunatenda dhambi hii?

2. Ni kwa nini dhambi ya upendeleo ni dhambi mbaya mno?

3. Ni matokeo gani mabaya au madhara tunayoyapata tunapotenda dhambi ya upendeleo?

4. Ni madhara gani wanayokutana nayo vikundi mbalimbali Wakristo wanapowatendea dhambi ya upendeleo au kuifanya dhambi hiyo mbele yao?

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

**IV. <u>Yak 2:14-26—Imani iliyo hai/inayotenda kazi</u>—*[14] Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yake yaweza kumwokoa? [15] Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, [16] na mtu wa kwenu akawaambia, "enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba," lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini? [17] Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake. [18] Lakini mtu atasema, "Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyesha imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu." [19] Wewe waamini kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka. [20] Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai? [21] Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? [22] Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale. [23] maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, "IBRAHIMU ALIMWAMINI MUNGU, IKAHESABIWA KWAKE KUWA NI HAKI;" naye aliitwa rafiki wa Mungu. [24] Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake. [25] Vivyo hivyo na Rahabu, yule kahaba naye, je! Hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipowakaribisha wajumbe, akawatoa nje kwa njia nyingine? [26] Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matedno imekufa.***

Sehemu hii ya kitabu pengine hutupa tafsiri iliyo wazi kuliko zote, ya imani ya kweli iokoayo ilivyo. Yakobo anaweka mkazo umuhimu wa "kazi" ikihusianishwa na imani ya mtu (*"imani pasipo matendo imekufa au haina faida,"* **mst.17, 20, 26;** *"mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake,"* **mst.24**). Watu wengine hufikiri kwamba hii iko kinyume na mkazo wa Paulo wa kuhesabiwa haki kwa imani peke yake (*"hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria,"* **Rum 3:20;** *"mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria,"* **Rum 3:28;** *"kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauawa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki,"* **Rum 4:5**).

Kwa hakika, Yakobo na Paulo hawatofautiani; wanakamilishana wao kwa wao. Hivi ndivyo ilivyo kwa sababu kadhaa:

- Paulo na Yakobo "wanazungumza kuhusu mambo tofauti: Paulo kuhusiana na tamko la haki yetu, na Yakobo kuhusiana na utendaji wa haki yetu. . . . Wote Paulo na Yakobo wanazungumzia haki ya mwenye dhambi mbele za Mungu, lakini fokasi ya Paulo ni namna ile hadhi inavyopokelewa katika hatua za awali na Yakobo namna ile hadhi inavyothibitishwa mbele za Mungu katika hukumu." (Carson na Moo 2005: 633) "Tofauti kati ya Paulo na Yakobo ipo katika ule mpangilio wa matendo na ile hali ya kupata badiliko: Paulo anakataa mabadiliko yatokanayo na matendo kabla ya kuongoka, lakini Yakobo anasihi kuhusiana na ule ulazima wa matendo mema baada ya kuongoka" (Moo 1985: 102). Burdick anaiweka hivi: "Yakobo alikuwa akipambana na imani ya juu juu ambayo haikuwa na matokeo kamili katika maisha ya mwamini anayoyakiri. Paulo, kwa upande mwingine alikuwa akipambana na ushikaji wa sheria—ile imani ya mtu ya kwamba anaweza kustahili kupata wokovu mbele za Mungu kwa matendo yake mazuri." (Burdick 1981: 185)
- Kwa sababu Yakobo na Paulo wanafokasi katika mambo tofauti au wanapambana na mawazo tofauti yasiyofaa kuhusianan na imani ya kweli ya Kikristo, wanatumia wazo la "imani peke yake" (ina maana, imani mbali na matendo) kwa maana nyingine, ingawaje wote wanakubaliana, kuhusiana na imani ya kweli ni nini: Yakobo anaelezea "imani peke yake" ya kwamba haiwezi kiukweli kuwa imani iokoayo; Paulo anatumia wazo la "imani peke yake" akiielezea imani ya kweli iokoayo: "Kwa Yakobo, 'imani peke yake' iko mbali kabisa na imani halisi ya Kikristo: hii 'imani peke yake' ni maneno tu bila vitendo (mst.15-16) au ujuzi wa kichwa bila ujuzi wa moyo (mst. 19). Hii si imani ya Kikristo. Na kwa upande wa Paulo hili halina ubishi; pia alikazia kwamba ni imani 'inayojidhihirisha yenyewe kwa upendo' hili lina uzito." (Moo 1989: 1157) "Ile aina ya imani ambayo Yakobo anasema 'imekufa' (hiyo ni, kama kitu ambacho kimefanyiki katika ufahamu tu, 2:14-17) hii si ile ambayo Paulo angeitambua kama imani halisi (yenyewe ni, 'imani itendayo kazi kwa upendo', Gal. 5:6)" (Marshall, Travis, na Paul 2002: 255).
- "Msimamo wa Paulo kuhusu 'imani na matendo' unahusiana na swali kwamba je Wakristo Wamataifa ni lazima watimize 'matakwa ya torati' – hasa hasa kutahiriwa, sabato na sheria za chakula. Mtazamo wa hoja ya Yakobo hauhusu kabisa Mataifa au maswala ya 'kuitimiza sheria'. . . . Kwa kweli wameingia katika mahojiano si wao kwa wao lakini na wapinzani tofauti – Paulo akiwa na wale ambao wangeamuru 'matendo ya sheria' kwa Mataifa, Yakobo akiwa na watu ambao wamekuwa goigoi katika maisha yao ya Kikristo" (Marshall, Travis, na Paul 2002: 255)." (Marshall, Travis, na Paul 2002: 255)

Carson na Moo wanawekea mkazo umuhimu wa kusikiliza mitazamo yote miwili ya Paulo na Yakobo:

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

"Unapokabiliwa na ushikiliaji mno wa sheria, kwa kujaribu kuweka msingi wa wokovu katika matendo mema ya mwanadamu, inahitajika kumsikiliza Paulo—kwa kuwa alikuwa na nguvu sana wakati wa Matengenezo. Lakini unapokabiliwa na falsafa ya unyenyekevu, yenye mwenendo ambao huona kwamba matendo mema hayana umuhimu kwa Wakristo, inahitajika kumsikiliza Yakobo—kwa kuwa alikuwa mwenye nguvu vilevile nyakati za Wesleys." (Carson na Moo 2005: 633) Sehemu hii ifuatayo inahusisha masuala muhimu ya imani na matendo:

1. Asili ya imani halisi, iokoayo. Swala lililo wazi la kifungu hiki ni asili ya imani ya kweli, iokoayo—si tu kufanya "matendo mema" kupata alama nzuri kutoka kwa Mungu au kujishindia nafasi yetu ya kwenda mbinguni. Kwa hiyo, **mst.14** unaanza, kwa uthabiti, kwa kuuliza swali: "Aina gani ya 'imani' ndiyo kweli iokoayo?" "Imani" ni zaidi ya "kuamini" kiakili katika kitu. "Imani" kwa hakika inahusisha vipengele muhimu vya mafundisho (angalia, mfano, **Matendo 2:22-24, 32-36; Rum 1:1-4; Rum 10:9; 1 Kor 15:1-8**). Lakini pia inahusisha kwa umuhimu ule ule tabia (angalia, mfano, **Efe 2:8-10; Yak 2:14-20; Math 28:18-20; Yohana 14:23-24**) na yenye matokeo au ya kujitoa (angalia, mfano, **Yohana 15:4-11; Yohana 15:12-15; Yohana 17:3; Yohana 21:15-17**) vipengele. Kwa maneno mengine, imani ya kweli, iokoayo inahusisha maisha yetu yote. Tunaona ya kwamba imani inahusisha maisha yetu yote katika **mst.19**. Hapo, mapepo yako sahihi *katika fundisho*: wanajua ya kuwa Mungu ni nani; wanajua ya kuwa Yesu ni Masihi. Lakini '*kuamini*' kwa mapepo hakukubadilisha maisha yao au tabia zao. Haikuwafanya wao wampende Yesu Kristo au wajitoe kwake. Wanaendelea kuwa wafuasi wa Shetani katika uasi dhidi ya Mungu ndani ya Kristo. Kwa hivyo, imani yao si imani halisi, iokoayo. Wamepotea na kuangamia.

2. Uhusiano kati ya imani na matendo. **mst.18** unaweka wazi ule uhusiano wa kweli uliopo kati ya imani na matendo unaposema, *"Nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu."* Swala si kuwa na imani *jumlisha* matendo au kuwa na imani *toa* matendo. Badala yake, imani ya kweli iokoayo siku zote huleta matokeo ya kubadilika kwa mfumo wa maisha, mabadiliko ya tabia, mabadiliko ya "matendo." Matendo yetu—jinsi tunavyoishi, kile tunachokiri ya kwamba tunakiamini—ni ushahidi wa uhalisia (au kukosa uhalisia) wa imani yetu. Wana Matengenezo walielewa waziwazi ile kanuni kwamba *tunaokolewa kwa imani peke yake, lakini imani ile iokoayo kamwe haiko peke yake*:

- *Martin Luther:* "Bila shaka imani lazima iwe ya kweli kutoka moyoni. Ni lazima iwe imani inayotenda matendo mema kwa upendo. Imani ikikosa upendo hiyo si imani ya kweli. . . . Kufikiri, 'Ikiwa imani hupata haki bila matendo, basi tusifanya cho chote,' ni kuidharau neema ya Mungu. Imani isiyotenda kitu si imani itupayo haki. . . . Ndani yake [imani itupayo haki] ina imani katika Mungu, nje yake ina upendo kwa wanadamu wenzetu." (Luther 1535: re. Gal 5:6)
- *John Calvin:* "Kadiri tunavyoendelea kuitaja imani peke yake katika swali hili, hatuifikirii imani iliyo kufa, ambayo haitendi kazi kwa upendo, lakini inashikilia imani kuwa ndiyo sababu pekee ya kupata haki. (Wagalatia 5:6; Warumi 3:22.) Kwa hiyo ni imani peke yake inayotupatia haki, na bado ile imani itupatiayo haki haiko peke yake: kama ilivyo kwamba ni joto la jua peke yake ambalo huleta joto duniani, na bado katika jua haliko peke yake, kwa sababu wakati wote limeunganika na nuru." (Calvin 1547: Antidote, Canon 11)
- *Muhtasari wa Fomyula ya Mapatano [Ukiri wa Imani ya Kilutheri]:* "Baada ya mtu kuhesabiwa haki kwa imani, hapo basi imani iliyo hai hutenda kazi kwa upendo, Gal. 5:6, ili kwamba matendo mema wakati wote hufuatana na imani iletayo haki, na kwa hakika hupatikana pamoja nayo, ikiwa ni ya kweli na iliyo hai: kwa maana kamwe haiwi peke yake, bali wakati wote iko pamoja na upendo na tumaini." (Epitome 1577: III.11)

Kumbuka, lile swali katika **mst.14** ambalo lilianzisha mjadala huu wote lilikuwa, *"Je! Ile imani yawezakumwokoa?"* Jibu la Yakobo liko wazi ni "Hapana." Anaiwekea uzito hoja hii katika **mst.17, 20, na 26** kwa kurudia, *"imani pasipo matendo imekufa (au haina faida)."* Wazi wazi kabisa anafananisha imani "iliyokufa" na imani "isiyofaa". Tunaona kwamba katika **mst.16-17** ambapo anauliza *"kuna faida gani ikiwa humsaidii mtu mwenye uhitaji wakati unao uwezo wa kufanya hivyo"* kisha anasema *"vivyo hivyo imani, ikiwa haina matendo imekufa."* Kwa maneno mengine, imani pasipo matendo *si imani iokoayo.*

3. Ni kwa nini imani na matendo vina uhusiano wa karibu sana. Imani ni kazi ya Roho Mtakatifu kuanzia mwanzo na wakati wote katika maisha yetu. Mpangilio wa mambo uko hivi: kwanza Roho Mtakatifu anatuhuisha (**Yohana 3:3, 5-8**); Anatenda kazi katika maisha yetu ili kutupa moyo mpya (**Yer 31:33; Ezek 11:19; 36:26**). Kama **Efe 2:8-9** inasema, *"[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; [9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."* Ni Mungu anayefanya kazi ya kuokoa, sio sisi. *Kisha*

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

*tunaitikia* kwa kuikiri imani yetu kwa Yesu Kristo na kuishi maisha mapya. Kama anavyoiweka Paulo katika **Efe 2:10**, *"Maana tu kazi yake, tuliubwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuende nayo."* Wokovu wetu hasa ni *"kwa ajili ya matendo mema"* ambayo Mungu aliyaandaa tuyatende. Mungu anahusika na maisha yetu katika ujumla wake wote. Wokovu wake uko kamili kwa sababu, kama **Rum 8:29** ituambiavyo. Sababu iliyo kubwa ya maisha yetu na ya Mungu kutuchagua na kutuokoa ni ili sisi *"tufananishwe na mfano wa Mwana wake [Yesu Kristo]."*

Ufunguo wa kuelewa uhusiano uliopo kati ya imani na matendo unaelezewa na Onesimus Ngundu: "Matendo ni ishara ya hali ya kiroho ya moyo wa mtu. . . . Hukumu haiko katika kuweka mizania kati ya matendo mema na mabaya. Badala yake, huonekana kama ushahidi usioweza kukosewa wa uaminifu wa moyo; huonyesha kuamini au kutokuamini, uaminifu au kutokuamini. Hukumu itadhihirisha kama uaminifu wa watu umekuwa kwa Mungu na Mwana Kondoo au kwa maadui wa Mungu." (Ngundu 2006: 1576) Swala ni *ile sababu itusababishayo* kufanya matendo mema. Sababu ya kawaida inayowasababisha watu kufanya matendo mema ni kujaribu kutendea kazi upendeleo wa Mungu. Hata hivyo, hali hiyo kwa hakika husababisha kutokuwa na uhakika na hofu, kwa sababu kamwe hatuwezi kuwa na uhakika kama "tunafanya vyakutosha" au tu "wazuri vya kutosha" Kutokana na injili, hata hivyo, hatumtii Mungu na kufanya matendo mema ili tupate upendeleo wake; tunamtii Mungu na kufanya matendo mema *kwa sababu yeye ameshatupa sisi upendeleo wake*! Kama mtume Yohana alivyosema, *"Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza"* (**1 Yohana 4:19**). Vivyo hivyo, hatutohitaji kuogopa au kuwa na mashaka lakini tunaweza *"tukikaribie kiti cha neema kwa <u>ujasiri</u>"* (**Ebr 4:16**), tukijua ya kwamba Yesu amesema *"Sitawapungukia kabisa wala sitawaacha kabisa"* (**Ebr 13:5**). Ni sahihi kwa sababu Mungu ndiye *"atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema"* (**Fil 2:13**) kwamba tunaweza kuutarajia ujio wa hukumu, tukijua ya kuwa matendo yetu "*yataonekana wazi ya kuwa yemetendwa katika Mungu"* (**Yohana 3:21**). Ndio maana, sasa na wakati wa hukumu ya mwisho, Mungu anahukumu na huwalipa watu na mataifa "sawasawa na matendo yao [au 'njia' au 'matendo']" (**Wamz 1:6-7; 9:22-24, 56-57; 2 Sam 12:9-12; 1 Fal 2:32-33; 20:35-42; 21:17-19; 2 Nyak 6:23, 30; Ayu 34:11; Zab 18:24; 31:23; 62:12; Mith 24:12; Mhu 12:13-14; Isa 59:18; Yer 17:10; 25:14; 32:19; Ezek 7:3, 8-9, 20, 23-24, 27; 9:10; 11:21; 16:43, 59; 18:30; 22:31; 24:14; 33:20; 35:6, 11, 15; 39:24; Hos 12:2; Yoel 3:5-7; Obad 15; Zek 1:6; Math 16:27; 25:14-46; Luka 12:47-48; Yohana 5:28-29; Rum 2:1-6; 12:19; 1 Kor 3:8, 11-15; 2 Kor 5:10; 11:15; Gal 6:7-8; Efe 6:8; Col 3:25; 2 Tim 4:14; Ebr 10:26-27; 1 Pet 1:17; 2 Pet 2:20-22; Yuda 14-15; Ufu 2:23; 14:13; 20:11-13; 22:12**). Yale matendo tutendayo—na ile sababu inayotusababisha kuyatenda—hudhihirisha hali ya moyo wetu.

4. <u>Mifano ya imani halisi, iokoayo.</u>

- *Mfano wa kwanza ni ule mfano wa kubuni katika* ***mst.15-16*** *wa mtu maskini mwenye uhitaji wa nguo au chakula.* Weka maanani kwanza jinsi kifungu hiki kinavyotiririka kutoka katika ule mjadala wa mtu maskini na mtu tajiri katika **mst.1-13**. Katika **mst.1-13**, yule mtu maskini alikuwa *hakupewa heshima*. Hapa, Yakobo anaanza na mfano wenyewe hasa wa mtu maskini na anaonyesha jinsi gani imani halisi hutenda kazi ili *kuwasaidia walio maskini* kutoka katika hali yake mbaya. Katika mfano huu Mungu anadhihirisha kwetu anavyovithamanisha na anavyovipa kipaumbele. Vile vile Yesu aliweka wazi kile ambacho kiko katika moyo wa Mungu wakati alipotuambia asili ya hukumu tutakayokutana nayo baada ya kufa katika **Math 25:31-46** (kondoo na mbuzi). Ile "imani" ya kondoo kamwe haikuwahi kuyabadilisha maisha yao au uhusiano wao na watu—hasa hasa wale ambao ni wahitaji. Kwa upande mwingine, ile imani ya kondoo ilipenya mioyoni mwao, katika fahamu na nafsi na kubadilisha mitazamo yao na maisha—na hata hawakugundua ni kwa kiwango gani walianza kuishi kama Yesu, kwa sababu viwango vya Yesu vimekuwa sehemu yao; viwango vya Yesu vimekuwa viwango vyao, kwa hiyo walipoanza kutenda kama yeye, haikuonekana kwao kondoo kuwa si kitu cha kawaida. Weka maanani kwamba Yakobo anazungumza kuhusu asili ya imani ya kweli, iokoayo katika **Yakobo 2**, anatumia mifano miwili kati ya ile ambayo inafanana na ile aliyoitumia Yesu katika **Mathayo 25**—mtu fulani ambaye anahitaji nguo na mtu fulani ambaye ana njaa. Tunapoona vitu kama hivi vimerudiwa, hiyo ni ishara ya kwamba Mungu anadhihirisha kile ambacho ni muhimu kwake. Ni *watu*—namna tunavyowatendea watu—hasa walio maskini, wenye uhitaji, waliokandamizwa, walio tengwa—hiyo huonyesha kama imani yetu iko hai au hapana.
- *Mfano wa pili wa imani iokoayo ni mfano wa Ibrahimu katika* ***mst.21-24***. Katika **mst.23** ile nukuu, *"Na Ibrahamu akamwamini Mungu, ikahesabiwa (au akamhesabia) kwake kuwa ni haki"*

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

inapatikana katika **Mwz 15:6** wakati Mungu alipomwahidi kupata mwana na akamwambia aangalie juu na kujaribu kuzihesabu nyota, kwa sababu hiyo ndiyo itakuwa idadi ya uzao wake itakavyokuwa kubwa kupitia mwana atakayepewa na Mungu. Ibrahimu alikuwa mzee, asiyeweza kupata watoto, lakini alimwamini Mungu, na Mungu akaihesabu ile imani kuwa haki. Yakobo anaendelea kuzungumzia kuhusu wakati ule ambapo Mungu alimwambia Ibrahimu amtoe Isaka dhabihu, mwana ambaye Mungu alimwahidia kumpa; Ibrahimu alitii, ingawaje Mungu alimwokoa Isaka (**mst.21**). Imani ya Ibrahimu katika ahadi ya Mungu—ya kuwa atapata mwana na uzao wake watakuwa wengi kama nyota za mbinguni—ilijaribiwa. Uhalisia wa imani ya Ibrahimu ulithibitishwa kwa yale aliyofanya, matendo yake. Mstari **22** unaelezea uhusiano wa ndani wa imani ya Ibrahimu (na yetu) na matendo: *"Imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake"* (angalia pia **Gal 5:6**). Moo anaelezea, "Imani ya Ibrahimu ilikuwa imani 'inayotenda kazi,' imani iliyo hai, imani ambayo haikuwa chanzo sana kama mwenza aliyekuwa naye wakati wote wa matendo yake. . . . 'Imani' si kitu ambacho Ibrahimu alikitendea kazi katika tukio moja tu; ilimhamasisha, ilimwongoza, na iliambatana na matendo yake." (Moo 1985: 112) Matokeo yake, Yakobo anaonyesha katika **mst.22** ya kwamba utii wa Ibarahimu "ulitimiliza" au "kukamilisha" imani yake. Neno lina maana "kutimiliza, kukamilisha kwa kufikia lengo lililokusudiwa" (Zodhiates 1993: *teleioō,* 1373).

Imani yetu haiwezi kukua au kufikia ukomavu bila matendo, bila kuiishi. Vinginevyo, ni kama mtoto aliyezaliwa akiwa mfu. Au ni kama mfano wa Yesu wa mpanzi wa mbegu: watu wengine wanalipokea lile neno, lakini Shetani analinyakua; wengine huanguka kwa sababu ya masumbufu; wengine wana neno linalosongwa kwa sababu ya wingi wa starehe (**Math 13:3-9, 18-23; Marko 4:3-9, 13-20**). Haya yote hayafikii ukomavu. Yote haya hayana faida kwa mpanzi. Ni aina moja tu ya mbegu ilianguka katika udongo mzuri, na kukua, na kuzaa matunda. Kundi hilo ni la wale wakomavu—wale waaminifu—wale ambao matendo yao yanaithibitisha ile kweli na uhalisia wa imani yao.

- *Mfano wa tatu wa imani iokoayo ni Rahabu katika **mst.25***. Rahabu anawaficha wale wapelelezi wawili na anapona kuuawa wakati wana wa Israeli walipouteka mji *si* tu mfano wa "kulipa jema kwa jema." Badala yake katika **Yoshua 2** inasema kwamba Rahabu aliikiri *imani* yake kwa kusema *"najua ya kuwa Bwana amewapa ninyi nchi hii"* (**Yosh 2:9**) na *"Bwana, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu, katika mbingu juu na katika nchi chini"* (**Yosh 2:11**). Ukweli wa kukiri kwake ulithibitishwa na kile alichokifanya kwa kuwaficha wale wapelelezi. Kwa hiyo, **Ebr 11:31** kwa dhahiri inaoanisha imani yake na matendo na kuitofautisha hiyo na ya wale ambao walikuwa "hawakutii" inaposema, *"Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani."*

Katika mifano hii yote, matendo ambayo Yakobo anayazungumzia ni yale ya nje, ushahidi unaoonekana wa imani unaotiririka kutoka katika imani yetu ya kiroho.

5. <u>Asili ya matendo yetu na uhusiano wake na imani.</u> Imani halisi, iokoayo imekusudiwa kutulazimisha sisi kutathmini vipaumbele vya maisha yetu na yaweza kutuongoza kutenda kinyume cha utamaduni na kwa namna zisiyozoeleka. Kwa mfano, mtazame Ibrahimu na Rahabu. Swali: Ibrahimu alikuwa yuko radhi kufanya nini? Jibu: Kumuua mwana wake. Swali: Rahabu alifanya nini hasa? Jibu: Alifanya uhaini. Tunahitaji kuelewa kitu fulani kuhusu mfano wa Ibrahimu. Kile ambacho Mungu alimwita Ibrahimu kukifanya kilikuwa cha kipekee sana, amri iliyo "bayana" aliyopewe Ibrahimu, sio amri ya "kiujumla" waliyopewa waaminio wote au Israeli. Lilikuwa ni tukio maalumu la kimfano katika historia ya ukombozi ambalo lilitangulia kama kivuli cha dhabihu ya Mungu ya Mwana wake pale msalabani.[8]

[8] Simulizi yote ya Ibrahimu na Isaka ni mfano wa kusulibiwa kwa Kristo. Kama vile Isaka alivyokuwa "*mwana wa pekee* [ina maani asiye kifani]" (**Mwz 22:2**), vivyo hivyo Kristo alikuwa *"Mwana wa pekee"* wa Mungu (**Yohana 3:16**). Kama vile ambavyo Isaka alibebeshwa kuni za kuichoma dhabihu (**Mwz 22:6**), vivyo hivyo Kristo alibebeshwa msalaba wake (**Yohana 19:17**). Kama vile Ibrahimu alisema kwamba *"Mungu atajipatia mwana-kondoo"* (**Mwz 22:8**) kwa ile dhabihu, hivyo Mungu alimtoa Yesu Kristo, *"Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu"* (**Yohana 1:29;** angalia pia **Ufu 5:6**). Kama ambavyo Isaka alikuwa mtii kwa mapenzi ya baba yake, hata katika kifo, vivyo hivyo Yesu alikuwa mtii kwa mapenzi ya Baba yake, hata mauti (**Math 26:39; Phil 2:8**). Kama ambavyo Isaka alikuwa "amekufa" kwa Ibrahimu katika muda wa siku tatu za safari yao (**Mwz 22:4**), vivyo hivyo, Yesu alikuwa kaburini kwa siku tatu (**Math 12:40; Luka 24:21**). Kama ambavyo Ibrahimu aliamini ya kwamba Mungu atamfufua Isaka kutoka kwa wafu (**Ebr 11:19**), vivyo hivyo, Yesu alifufuliwa kiuhalisia (**Math 28:1-6; Marko 16:1-13; Luka 24:1-6; Yohana 20:1-28**). **Ebr 11:19** (NASB) pia inasema kwamba Ibrahimu alimpokea Isaka tena *"kama mfano."* Wengine wamegundua ukweli pia katika mfano wa yule kondoo kuhusiana na ukweli ya kwamba alikuwa *"amenaswa pembe zake katika kichaka"* (**Mwz 22:13**).

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Maandiko mengine yanadhihirisha wazi wazi ya kwamba Mungu anapinga—na kwa dhahiri anakataza—kumwaga damu isiyo na hatia (angalia **Kut 20:13; Mith 6:16-17**). *Kanuni* ya simulizi ya kipekee ya Ibrahimu ambayo inatenda kazi kwetu pia *si* "uende ukawachinje watoto wako," lakini "uwe tayari kumtumikia Mungu kwa kila kitu ambacho unakipenda sana moyoni mwako." Mfano wa Rahabu, hata hivyo, unajulikana sana: serikali inapotutaka tufanye vitu ambavyo viko kinyume na imani yetu, basi, kama Petro alivyosema, *"Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu"* (**Matendo 5:29**). Kanuni hii inaturudisha nyuma hadi mwanzoni mwa Israeli wakati wazalishaji wa Kimisri walipoacha kumtii Farao na wakakataa kuwaua watoto wa kiume wa wana wa Israeli kwa sababu "walikuwa na hofu ya Mungu" (**Kut 1:15-21**).

Hii mifano ya Ibrahimu na Rahabu ni ushahidi kwamba yale "matendo" ambayo Yakobo anayazungumzia si tu "matendo mema" au hata "matendo ya hisani" lakini ni matendo ya *utii* (angalia **Yohana 14:15, 21, 23; 15:12-17; 1 Yohana 5:3; 2 Yohana 6**). Mungu anaweza kuweka ndani yetu maeneo magumu na kuijaribu imani yetu. Utii kwa Mungu unaweza kuleta matokea ya sisi kupata mateso kwa ajili ya imani yetu na hata kuuawa (angalia **Math 10:22; 24:9; Yohana 15:20; Ebr 11:35-40**). Haya yameshatokea katika historia yote, kuanzia na mitume wa kwanza ambao waliwekwa gerezani na kuchapwa kwa ajili ya kuhubiri habari za Yesu lakini *"walifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo"* (**Matendo 5:41**) Ni katika nyakati za mifadhaiko, upinzani, hali ngumu, na majaribu ndipo kilichomo ndani yetu kinaweza kudhihirika. Ni nyakati na matukio kama hayo ndiyo hudhihirisha ni nani *hasa* ndiye Bwana wetu: Je ni Yesu, au ni hali yetu ya kuwa salama?

## MASWALI YA KUJADILI

1. Unaulinganishaje mkazo wa Paulo kuhusu kuhesabiwa haki kwa imani peke yake pasipo matendo (angalia Rum 3:20, 28; 4:5) na kauli ya Yakobo kwamba imani pasipo matendo imekufa (angalia Yak 2:17, 20, 26)?

2. Kwa mujibu wa Yak 2:14-26 kuna uhusiana gani kati imani na matendo, na ni kwa nini imani na matendo huhusiana kwa karibu? Kuiweka kwa namna nyingine, imani ya kweli iokoayo in amaana gani na ikoje?

3. Yakobo anaposema kwamba imani pasipo matendo "imekufa," hiyo ina maana gani?

4. Jadili hii mifano mitatu ambayo Yakobo anaitoa (angalia Yak 2:15-16 [maskini ambaye ana shida ya nguo au chakula], Yak 2:21-24 [Ibrahamu], na Yak 2:25 [Rahabu]). Kuna kanuni gani katika mifano hii? Ni kwa namna gani mifano hii ina maana na inaweza kutumikaje siku za leo?

**V. Yak 3:1-12—Dhambi ya kutotawala ulimi—*Ndugu zangu, msiwe waalimu wengi, mkijua ya kuwa mtapata hukumu kubwa zaidi. [2] Maana twajikwaa sisi sote pia katika mambo mengi. Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu. [3] Angalieni, twatia lijamu katika farasi, ili watutii, hivi twawageuza mwili wao wote. [4] Tena angalieni merikebu; ingawa ni kubwa kama nini, na kuchukuliwa na pepo kali, zageuzwa na usukani mdogo sana, kokote anakoazimia kwenda nahodha. [5] Vivyo hivyo ulimi nao ni kiungo kidogo, nao hujivuna majivuno makuu. Angalieni jinsi moto mdogo uwashavyo msitu mkubwa sana. [6] Nao ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi, huuwasha moto mfulizo wa maumbile, nao huwashwa moto na jehanamu. [7] Maana kila aina ya wanyama, na ya ndege, na ya vitu vitambaavyo, na ya vitu vilivyomo baharini, vinafugiki, navyo vimekwisha kufugwa na wanadamu. [8] Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga; ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti. [9] Kwa huo twamhimidi Mungu Baba yetu, na kwa huo twawalaani wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu. [10] Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, hiafai mambo hayo kuwa hivyo. [11] Je! Chemchemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu? [12] Ndugu zangu, Je! Mtini waweza kuzaa zeituni au mzabibu kuzaa tini? Kadhalika chemchemi haiwezi kutoa maji ya chumvi na maji matamu.***

Sehemu hii ya kitabu hiki, ambayo fokasi yake ni yale ambayo watu husema au ulimi, inaweza kugawanywa katika sehemu ndogo tatu: **mst.1-2**—wajibu wa walimu; **mst.3-6a**—nguvu kubwa ya ushawishia iliyomo katika ulimi; na **mst.6b-12**—ule uwezo wa kuharibu na upotovu wa ulimi:

---

Augustine alisema, "Je, sasa, alifanya nini [yule kondoo] anamwakilisha Yesu, ambaye, kabla hajatolewa, aliwekewa taji ya miiba?" (Augustine 1950: 16.32)

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

1. **mst.1-2**—<u>Wajibu wa walimu.</u> Yakobo anaanza sehemu hii inayohusu kusema (ulimi) kwa kuzungumza kuhusu walimu, kwa sababu kufundisha ni huduma iliyo muhimu sana ndani ya kanisa (angalia **Matendo 13:1; Rum 12:6-7; 1 Kor 12:28; Efe 4:11-12**). Ikifanywa kidhaifu au kwa dhamira zisizosahihi, walimu wanaweza kuleta upotovu ndani ya kanisa na kuwapoteza wengi. Kwa sababu ya wajibu huu mkubwa wa kufundisha neno la Mungu kwa usahihi, Yakobo anawaonya walimu *"watapata hukumu kubwa zaidi."* Onyo hilo linaendana na kanuni ambayo aliisema Yesu katika **Luka 12:48**: *"Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi; kwake huyo watataka na zaidi."* Katika **Marko 12:38-40** Yesu aliitumia kanuni hiyo kwa waandishi wa Kiyahudi ambao katika nafasi yao ya mamlaka walipenda sana kuvaa kanzu ndefu, kusalimiwa kwa heshima sana wawapo sokoni, na kukaa katika viti vya mbele katika sinagogi na viti vya heshima katika sherehe. Walitumia vyeo vyao *"kula katika nyumba za wajane."* Kwa maneno mengine, kama Victor Babajide Cole anavyotoa ufafanuzi, "Waliwawinda wasiojua na wadhaifu, wakiwakilishwa na wajane ambao hawakuweza kujitetea. Mbaya zaidi, walifunika uovu wao na maombi ya kujifanya, marefu ya hadharani (**12:40**). Yesu alionya ya kwamba watu watendao kwa namna hii watapata hukumu kali zaidi. Cha kusikitisha, onyo hili bado litatuhusu kiukweli katika kizazi chetu cha sasa. Sote, watu wa Mungu na watumishi wa Injili lazima wawe makini wasiangukie katika tabia kama hizi ambazo kwa hakika zitawashushia ghadhabu ya Mungu." (Cole 2006: 1193)

Sababu ya onyo la Yakobo katika **mst.1** inapatikana katika **mst.2** ambao unaanza na lile neno "maana" (inamaanisha, "kwa sababu"). "Mwalimu anajiweka yeye mwenyewe katika hatari kubwa ya hukumu kwa sababu kifaa kikubwa cha huduma yake ndicho pia kiungo cha mwili ambacho ni kigumu zaidi kukitawala: ulimi" (Moo 1985: 120). Mawazo ya Yakobo katika **mst.2** hayaishii kwa walimu tu lakini yanahusisha watu wote, kwa kuwa *"twajikwaa sisi sote"* na *"mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu"* (ambapo hayupo hata mmoja). Hili linatukumbusha kwamba dhambi iko kila mahali, hata miongoni mwa waaminio. Kwa hiyo mstari huu unatumika kama mpito wa kifungu kidogo kinachoanzia katika **mst.3** kuhusiana na ushawishi mkubwa wa ulimi. Yakobo anatupa uhusiano uliopo kati ya kile tunachosema na kile tunachofanya. Maoni yake ni kwamba "kwa kuwa dhambi za ulimi ndizo zilizo ngumu zaidi kuzishinda, ye yote ambaye angeweza kuutawala ulimi wake kwa hakika atakuwa na uwezo wa 'kuutawala mwili wake wote'—inamaanisha, ataweza kuuzuia usitumiwe kama chombo cha dhambi" (Burdick 1981: 187). Kwa kuwa hitimisho la "tunda la Roho" lililoorodheshwa na Paulo katika **Gal 5:22-23** ni "kiasi," Vivyo hivyo Yakobo anasema kwamba ikiwa tutaweza kuwa na kiasi katika ulimi wetu, tutaweza kuwa na kiasi katika kila eneo la maisha yetu.

2. **mst.3-6a**—<u>Ushawishi wenye nguvu wa ulimi.</u> Katika **mst.3-6a** Yakobo anatumia mifano mitatu kuonyesha kwamba, ingawaje ulimi ni kiungo kidogo katika mwili, una ushawishi mkubwa juu ya maisha yetu. Analinganisha ulimi na lijamu katika kinywa cha farasi ambayo inaweza kuongoza mwendo wote wa farasi mkubwa na mwenye nguvu, na usukani mdogo ambao unaweza kuongoza mwelekeo wa merikebu kubwa, na cheche ndogo ambayo inaweza kuchoma msitu mkubwa. Moo anatamatisha: "Kwa hiyo ulimi unaweza kuamua hatima ya mtu. Mwamini anapotiisha ulimi wake kwa makini, inaweza kudhaniwa ya kwamba anaweza pia kuyaongoza maisha yake yote katika kusudi la kiungu lililokusudiwa: yeye ni 'mtu mkamilifu' (mst.2). Lakini ulimi usipotawaliwa, ingawaje wenyewe ni mdogo, ni dhahiri mwili wote utakuwa hautawaliki na hauna nidhamu pia." (Moo 1985: 122)

Ule mfano wa moto mwishoni mwa **mst.5** na mwanzoni mwa **mst.6** pia ni mpito kuelekea kifungu kidogo kinachofuata kinachohusu nguvu ya uharibifu na upotovu wa ulimi. Hili linaonekana katika utofauti uliopo kati ya mfano wa moto na farasi na merikebu. Usukani mdogo, kama ulimi, unatumika kuendesha vyombo vikubwa na kuvifanya viende katika uelekeo ule ambao mtu anataka viende, lakini moto wa msituni hautawaliki. Zaidi ya hapo, katika **mst.6a** Yakobo si tu anasema kwamba *"ulimi ni moto"* lakini anaendelea kuuita *"ule ulimwengu wa uovu."*

3. **mst.6b-12**—<u>Nguvu ya uharibifu na upotovu wa ulimi.</u> Nguvu ya uharibifu ya ulimi imewekwa wazi na kauli nne katika **mst.6**:

- *Ulimi ni moto*. Hii hurudi nyuma hadi sehemu ya mwisho ya mst. 5 ambao unazungumzia kuhusu jinsi vile ambavyo moto mdogo unaweza kuwasha msitu mkubwa.
- *Ulimi unanajisi mwili wote*. Yakobo anaonyesha kwamba ulimi hutekeleza kinyume cha *"dini iliyo safi, isiyo na taka"* (**Yak 1:27**). Neno lililotafsiriwa "unajisi" katika **mst.6** maana yake hasa ni "kutia madoa" au "kuchafua" (Kiyunani = *spilousa*). Linatokana na neno lililotumika katika **1:27** ambalo linasema kwamba dini iliyo safi inahusisha kujilinda mwenyewe *"<u>usichafuliwe</u> [Kiyunani = aspilon] na dunia."* Katika **mst.6**, Yakobo anaposema kwamba ulimi *"hutia mwili wote unajisi,"* kwa asili anasema kwamba "zile dhambi zinazotendwa na ulimi husambaza uchafu wa kiroho katika

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

mtu mzima" (Moo 1985: 125).

- *Ulimi huwasha moto wa mwendo wa maisha yetu*. Kauli hii huenda zaidi ya kukubali kwamba ulimi huyaathiri maisha ya mnenaji tu hadi kusema kwamba "ile nguvu kubwa ya uharibifu ya ulimi huathiri wanadamu wote, kuanzia mwanzo hadi mwisho, na katika mazingira yake yote" (Ibid.: 125-26).
- *Ulimi umewashwa moto na jehanamu*. Kauli hii inatujulisha ni wapi ulimi unapata ile nguvu yake kubwa ya uharibifu: kutoka jehanamu. Kwa kusema kwamba ulimi *"unachochewa moto na jehanamu,"* Yakobo anasema kwamba Shetani ndiye chanzo cha maneno mabaya na cha uwezo wa sisi kujiharibu wenyewe, wengine, na mahusiano yetu kwa yale tunayosema. "Jehanamu" inatumika hapa kama ufupisho wa kumuelezea Shetani, kwa kuwa ule moto wa milele wa jehanamu *"alioandaliwa tayari ibilisi na malaika zake"* (**Math 25:41**). Hii ni sawa na jinsi Mathayo mara kwa mara anatumia kufungu cha maneno *"ufalme wa mbinguni"* kueleza kuhusu ufalme wa Mungu (angalia mfano, **Math 3:2; 4:17; 5:3, 10, 19; 7:21**). Zaidi ya hayo, Shetani *"hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo."* (**Yohana 8:44**)

Upotevu wa ulimi unaonekana katika **mst.6a, 7-12**. Tunaona kwanza katika **mst.6** na **8** ambayo huelezea asili potofu ya ulimi. Mstari **6** huuita ulimi *"ulimwengu wa uovu,"* na **mst.8** unaongezea kwamba ule ulimi *"ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti."* Hii iko sawa na kile alichosema Yesu katika **Math 15:11, 18-19**, *"Sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi; bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi . . . Bali vitokavyo kinywani vyatoka moyoni; navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi. Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano."* Ulimi unadhihirisha ile hali ya mwanadamu ya kuharibika, kuanguka, ya dhambi.

Pili, tunauona upotevu wa ulimi katika **mst.7-12**. Mistari wa **7-8** inasema kwamba, licha ya uwezo wetu wa kufuga wanyama, hatuwezi kuufuga ulimi. Kisha mistari wa **9-10** huonyesha kwamba hali ya kukosa msimamo ni elementi ya upotevu wa ulimi: kutoka katika kinywa kimoja hutoka Baraka na laana. Mwisho, **mst.11-12** hufananisha ulimi na chemchemi, mtini na maji ya chumvi. Kigezo chake ni kwamba vitu hivi vingine vyote hutenda kazi kwa kuifuata asili yao: chemchemi haitoi maji matamu na machungu; mtini huzaa tini sio zabibu; maji ya chumvi hayatoi maji matamu. Vivyo hivyo, Mungu ametukusudia sisi tumpende na tuwapende wengine na ametupa uwezo wa kufanya hivyo. Hata hivyo, badala ya kudumu katika kumpenda Mungu na kuwapenda wengine, tunakuwa kama chemchemi ambayo inatoa maji matamu ma machungu, au kama mtini ambao unazaa tini na zabibu. Kama navyosema Yakobo, *"Ndugu zangu haifai mambo haya kuwa hivyo"* (**mst.10**). Sababu inayofanya hii iwe muhimu sana tunaipata kutoka kwa kauli ya Yakobo ambaye alisema, *"Kwa matunda yake mti hutambulikana"* (**Math 12:33**). Swala ni la kiroho: hinachotoka vinywani mwetu hudhihirisha hali ya kiroho ya mioyo yetu. Hatimaye, kwa hiyo, ulimi wetu unadhihirisha kama tumeokoka au hatujaokoka.

## MASWALI YA KUJADILI

1. Katika Yak 3:1 walimu wanaonywa ya kwamba kama walimu "tutapata hukumu kubwa."
   - Ni kwa nini ni sawa na haki kwamba walimu wapate hukumu kubwa?
   - Ni njia gani tofauti ambazo kwazo walimu watapata hukumu kubwa?

2. Katika kifungu hiki, moja ya dondoo za Yakobo ni kwamba ulimi una ushawishi mkubwa katika maisha yetu. Jadili njia mbalimbali tofauti ambazo kwazo ulimi una ushawishi mkubwa na mifano.

3. Yakobo pia anadokeza kwamba ulimi una uwezo mkubwa wa kuleta uharibifu. Jadili njia tofauti ambazo kwazo ulimu ni mharibifu, weka na mifano.

4. Ni kwa namna gani Wakristo wanaweza kutawala kile kinachomtoka midomoni mwao? Je kuna mbinu ambazo umezipata za kukusaidia kutawala kile kinachotoka kinywani mwako?

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

**VI. <u>Yak 3:13-18—Hekima itokayo juu dhidi ya ile isiyotoka juu</u>—*[13] N'nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aonyeshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri, katika upole wa hekima. [14] Lakini, mkiwa na wivu wenye uchungu na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uongo juu ya kweli. [15] Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani. [16] Maana hapo palipo na wivu na ugomvi ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya. [17] Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki. [18] Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani.***

Katika sehemu hii, Yakobo anaonyesha tofauti kati ya hekima ya mbinguni na duniani. Katika **mst.13** Yakobo anatuonyesha kwamba hekima huifanania imani (angalia **Yak 2:18**): kama vile imani ni *kutendea kazi ulichoamini*, vivyo hivyo hekima ni *kutendea kazi maarifa*. Moo anaiweka hivi: "Hekima ya kweli, kama ilivyo imani halisi, ni muhimu, yenye ubora wa kimatendo ambayo ina kiwango kikubwa (au zaidi) kinachohusiana na namna tunavyoishi ikiendana na vile tunavyofikiri au kusema" (Moo 1985: 132). Yakobo anaweka ulinganishi ufuatao:

| *Hekima ya Kidunia* | *Hekima ya Mbinguni* |
|---|---|
| **Inakotoka** | **Inakotoka** |
| Ya dunia hii, ya kawaida (si ya rohoni), ya kipepo (**mst.15**) | Inatoka juu (mbinguni) (**mst.15, 17**) |
| **Asili na Matunda** | **Asili na Matunda** |
| Wivu, ubinafsi, kukosa utaratibu, kila kitu kilicho kiovu (**mst.16**) | Tabia njema, upole (**mst.13**), safi, ya amani, tulivu, inasikiliza, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki, haki, amani (**mst.17-18**) |

Tambua kwamba hekima ya kidunia ni ya ubinafsi, wakati ambapo hekima ya mbinguni inajihusisha na wengine. Ulinganishi wa Yakobo wa hekima ya kidunia na hekima ya mbinguni uko sambamba na ulinganishi wa Paulo wa mwili na Roho katika **Gal 5:16-26**.

## <u>MASWALI YA KUJADILI</u>

1. "Hekima" ni nini?

2. Watu wengi wana akili na wana elimu kubwa, lakini si "wenye hekima," Jadili tofauti yake.

3. Je, hekima inaweza kufundishwa, ikiwa ndivyo, ni kwa namna gani?

**VII. <u>Yab 4:1-4—Dhambi iliyo ndani na madhihirisho yake ya nje</u>—*Vita vyatoka wapi, na mapigano yatoka wapi? Si humu, katika tamaa zenu zifanyazo vita katika viungo vyenu? [2] Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! [3] Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu. [4] Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.***

Sura ya **3** inaishia kwa kuonesha tofauti iliyopo kati ya hekima ya kweli na hekim ya uongo. Sasa sura ya **4** inafuatia kutoka hiyo kwa kujadili asili ya wale ambao hutenda kwa misingi ya hekima isiyo kweli. Uzito wa hili unaonekana katika lugha kali anayotumia Yakobo. Watu kama hao wana "magomvi na migogoro" miongoni mwao; anasa zao "hupigana vita" ndani yao wenyewe; "wanatamani" na "kuua"; wana "wivu" unaowasababisha wao "kupigana na kugombana"; wana "nia mbaya"; "ni wazinzi"; ni "maadui wa Mungu." Jambo la kusikitisha sana ni kwamba haya wameandikiwa wale ambao hujiita Wakristo (angalia **Yak 2:1**). Mistari hii huibua maswala kadhaa:

1. <u>**mst.1-2**—Chanzo cha matatizo yetu.</u> Katika mistari hii Yakobo anaweka wazi kwamba chanzo cha migogo yetu na ugomvi ni ubinafsi wetu. Kwa hiyo, anazungumza kuhusu anasa zetu, tamaa mbaya, na wivu kama chanzo cha matatizo yetu na wengine. Mizizi ya haya yote ni ubinafsi. Katika **1:14**, katika kuzungumza chanzo cha dhambi kwa ujumla, Yakobo vile vile alishasema kwamba *"kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa."* Hapa fokasi yake iko kwenye migogoro inayohusisha watu inayosababishwa na anasa za ubinafsi, tamaa mbaya, na wivu. Hiyo migogoro ya watu ni ushahidi kwamba *hatuitii* ama amri ya kwanza na iliyo kuu, *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote"* (**Math 22:36**), na pia hatuitii amri ya pili, *"Mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Math 22:39**).
2. <u>**mst.2**— "Kuua."</u> Mstari pili unasema, *"Mwatamani wala hamna kitu, kwa hiyo mwaua."* Kwa kuwa Yakobo anawaandikia Wakristo, ni wazi hamaanisha kwamba Wakristo wanauana wao kwa wao hasa.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Badala yake, "ni katika muktadha wa maneno makali kama vile *polemoi* ('vita') [imetafsiriwa hapo juu kama 'ugomvi'] na *machai* ('mapambano') [imetafsiriwa hapo juu kama 'migogoro'], inaonekana ni bora kuchukua *phoneuete* ('unaua') ni kama kutia chumvi kwa sababu ya chuki. Hili pia hutatua lile tatizo ambalo ni kama si kubwa sana la mpangilio wa maneno. Kusema 'Unachukia na kutamani' ni utaratibu ulio wa kawaida zaidi badala ya kusema 'Unaua na kutamani.' Zaidi ya hayo, Mathayo 5:21-22 na 1 Yohana 3:15 inaonyesha kwamaba kuchukia ni sawa na kuua." (Burdick 1981: 193) Kwa nyongeza, Yakobo anatambua kwamba, kwa kuwa ugomvi, migogoro, na vita tayari vipo katika jamii ya Wakristo, wakiendelea kuhamasika kutamani, kuona wivu, na kuwa na ubinafsi hawataweza kuepuka kuingia katika kupigana hasa na kuua.

3. **mst.2b-3**—Maombi. Baada ya kuongea kuhusu ubinafsi, tamaa mbaya, na wivu ambavyo vimesababisha migogoro, ugomvi, na vita, Yakobo anasema, , *"Wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi!"* Kisha hapo hapo anaongezea, *"Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu."* Kimsingi. "maombi" ya kibinafsi, wakati mtu fulani anaomba vitu kwa Mungu kwa ajili ya sababu za kibinafsi ili akavitumie katika tamaa zake na anasa, ni sawa na kutoomba kabisa! Kwa kweli, mbaya kuliko hivyo. Anasema kwamba hata maombi kwa kweli yanatumiwa kama chombo cha kutosheleza tamaa zetu.

Hili ni swala muhimu leo, hasa kutokana na kuzuka kwa kile kinachoitwa "injili ya mafanikio," ambayo inashikilia kwamba Mungu anataka sisi tuwe na utajiri mkubwa wa vitu na ya kwamba kuwa na utajiri mkubwa wa vitu ni ishara kwamba tuna uhusiano mzuri na yeye na tuna kibali cha Mungu. Katika mafundisho ya mafanikio, imani na maombi vimetafsiriwa upya: "Kuamini moyoni kumefunganishwa na kukiri kwa kinywa ili kuleta uhalisia. 'Unapokea katika maisha haya kwa kule kusema tu kwa kinywa chako. Neno katika kinywa chako ni imani yako inenayo. *Maneno usemayo ndio kile unachoamini.* Maneno yako yanaweza kukusaidia au kukuangamiza. Yanakuletea afya au magonjwa. Maneno yako yanaamua kama utaishi katika utele au uchache.'" (Sarles 1986: 347-48, akimnukuu Gloria Copeland). Mafundisho haya ni potofu kabisa. "Katika mtazamo wa namna hii imani ni aina fulani ya uchawi, pamoja na lile neno unalokiri kama tabano. Mantiki ya ndani ya fikra za mafanikio hutoa hoja kwamba kwa kuwa mtu ni kiumbe ambaye ni mfano wa kama mungu, maneno yake, yanaposemwa kwa imani, yanakuwa na nguvu ile ile halisi kama ya Mungu. Lakini hii dhana ya ukiri wa mwanadamu ni ya kichawi si ya kiroho." (Ibid.) Gordon Fee anaongezea, "Katika msingi wake fundisho potofu [la] mafanikio hutoa theolojia ya mtu kijitazama yeye, badala ya kumtazama Mungu. Hata ingawaje mtu ataambiwa mara kwa mara kwamba ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu kwamba tunapaswa kufanikiwa, mvuto siku zote uko katika ubinafsi wetu na nia ya yetu ya kujitosheleza." (Fee 1984: 42-43) Mvuto wa injili ya mafanikio kwa ubinafsi wetu hauna kitu zaidi ya kutuvuta katika ulafi na kutamani. Mbali na kuweka imani katika matendo, Biblia inasema kwamba mtu mwenye kutamani *"ni mwabudu sanamu"* (**Efe 5:5**), na mlafi *"huishia kwenye ibada ya sanamu"* ambayo huleta *"ghadhabu ya Mungu"* (**Kol 3:5-6**).

Ni kweli, haswa, kwamba Yesu alisema, *"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa"* (**Math 7:7**) na *"Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea."* (**Math 21:22**). Wengine wameitumia mistari hiyo kama hoja ya kuunga mkono theolojia isemayo "ikiri na uidai"—ina maana, waaminio wanaweza kuwa na kitu chochote kile ambacho wanakiomba, na sababu pekee inayofanya wasipokee hivyo vitu ni kukosa imani. Hata hivyo, **1 Yohana 5:14-15** inatuambia kwamba maombi yanayojibiwa sharti yaombwe *"sawa sawa na mapenzi yake"* (sio mapenzi yetu sisi). Hata wakati huo wa nyuma, Mungu alikataa kuwapa maombi yao mtume Paulo (**2 Kor 12:7-9**) na Bwana Yesu mwenyewe (**Luka 22:41-42**)—pamoja na kwamba hakuna mmoja wao ambaye alikuwa na "upungufu wa imani." Mwisho wa haya yote Mungu ndiye mwenye mamlaka yote, na tunahitaji kukumbuka hilo tunapoomba. **Jas 4:3** anaweka wazi hoja ya kwamba sababu yetu ya kuomba kitu ni muhimu sana. Maombi yetu hudhihirisha ikiwa tegemeo letu hasa liko kwa Mungu na ikiwa tunataka kweli mapenzi yake katika maisha yetu, au ikiwa tegemeo letu hasa liko katika vitu na kunufaika kwetu. Ikiwa hili la mwisho ndilo lenyewe, tunadhihirika sisi wenyewe kuwa waabuduo sanamu ndani ya mioyo yetu—na Mungu hatawabariki waabudu sanamu.

4. **mst.4**—Uhusiano wetu na Mungu. Mstari **4** unaweka muhuri juu ya mjadala kuhusu ubinafsi, tamaa, wivu na maombi. Tatizo la watu wengi wale ambao Yakobo alikuwa akiwaandikia—na tatizo la wafuasi wengi wa injili ya mafanikio na wengi wetu leo—ni kwamba walikuwa na wao ni "wa dunia" na ukijumlisha na kuwa "duniani." Kwa maneno mengine, vile wanavyovithamanisha, wanavyovipa umuhimu mkubwa, na matakwa huzingatia vile dunia inavyovithamanisha, inavyovipa umuhimu mkubwa na inavyovitaka. Maneno yao huwazungukia wao wenyewe, si kuhusu Mungu naYesu Kristo.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Yakobo anapowaita watu wabinafsi, waliojaa tamaa "wazinzi" inaonyesha kwamba, moyoni, uhusiano wa mtu na Mungu uko hatarini. Sababu ni kwamba "wazinzi" ni lugha ya mfano ikimaanisha kukosa uaminifu kiroho. Ni neno lililo wazi sana na la kushtusha lililokusudiwa kumfanya msomaji aamke kutoka katika hali yake na kumpeleka katika hali ya kweli ya kiroho. Dhana ya uzinzi wa kiroho bila shaka imechukuliwa kutoka AK (cf. Hos 2:2-5; 3:1-5; 9:1)." (Burdick 1981: 193) Sisi, kanisa, ni bibi arusi na mke wa Kristo (**Efe 5:23, 32; Ufu 19:7; 21:2, 9**). Bwana, Bwana arusi wetu, anatutaka na ana haki ya kupata kipekee uaminifu na ukweli wetu wote, kama vile mwenza ye yote anavyotaka na anastahili kupata uaminifu wote kutoka kwa mwenzi weka.

Yakobo hangeweza kuwa wazi zaidi ya hapo au kuonyesha zaidi kuhusiana na uzito wa hili anaposema, *"Ye yote anayetaka kuwa rafiki wa dunia amejifanya yeye mwenye adui wa Mungu."* Kilicho muhimu kwetu na kile tunachokitaka zaidi, kama inavyoonyesha katika maombi yetu, kina athari za milele. Mambo haya hudhihirisha hali halisi ya moyo wetu. Na tunapaswa kukumbuka wakati wote kwamba *"Bwana huutazama moyo"* (**1 Sam 16:7**). Kama alivyofanya katika katabu hiki chote, kifungu hiki kinagonga katika moyo wa imani ya kweli dhidi ya imani ya uongo. Hili ni swala ambalo huenda nyuma mbali sana hadi **Mwz 3:15**: *"Nami nitaweka uadui kati . . . uzao wako [ina maana, Shetani, mungu wa dunia, na wafuasi wake wote] na uzao wa mwanamke [ina maana, Yesu, Mungu wa kweli wa dunia, na wote wanaomwamini]."* Wakati wote imekuwa hivyo: dunia dhidi ya ufalme wa Mungu; imani dhidi ya matendo. Mtazamo huu wa uhalisia, ya kwamba kuna njia mbili tu—njia ya Mungu na njia ambayo inapingana na Mungu—inaonekana katika Biblia yote (angalia, mfano, **Zab 1; 73; Math 7:13-20, 24-27; 1 Kor 2:14-15**). Huenda itapata kufikia kilele cha kuonekana kwake hivyo katika kitabu cha Ufunuo wakati wanadamu wote (*"kila kabila na jamaa na lugha na taifa"*) watakapoonekana wakiwa katika sehemu moja kati ya kambi mbili, ambazo zinapingana: dunia (**Ufu 11:9; 13:7; 14:6**; angalia pia **17:15**), au kanisa (**Ufu 5:9; 7:9**); wale wakaao dunianih (**Ufu 3:10; 6:10; 8:13; 11:10; 13:8, 12, 14; 14:6; 17:2, 8**), au wale ambao ni raia wa mbinguni (**Ufu 6:9, 11; 7:9-10; 11:12; 12:10; 14:1-3; 15:2-4; 19:1-9, 14; 20:4-6**); wale ambao wanamwabudu yule mnyama (**Ufu 13:3, 4, 8, 12, 15; 14:9, 11; 19:20**), au wale wanaomwabudu Mwana kondoo (**Ufu 4:8-11; 5:9-14; 6:9; 7:9-17; 11:15-18; 12:11, 17; 14:4, 12; 15:2-4; 17:14; 19:5-9; 20:4; 21:9; 22:3**); wale ambao wana alama ya mnyama (**Ufu 13:16-17; 14:9, 11; 19:20**), au wale wenye muhuri wa Mungu (**Ufu 7:3; 9:4; 14:1; 22:4**); wale ambao majina yao hayakuwahi kuandikwa katika kitabu cha uzima (**Ufu 13:8; 17:8; 20:15**), au wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima (**Ufu 3:5; 21:27**); wale ambao ni sehemu ya "mji mkuu" (**Ufu 11:8; 16:19; 17:18; 18:10, 16, 18, 19, 21**), au wale ambao watakuwa sehemu ya "mji uliopendwa" (**Ufu 20:9**). Hakuna "kutokuwa upande wowote" au chaguo la tatu.[9]

## MASWALI YA KUJADILI

1. Katika mistari hii ni kitu gani ambacho Yakobo anakitaja kuwa ni chanzo cha dhambi zetu, ugomvi, na migogoro?

2. Katika Yak 4:2-3 Yakobo anatoa kauli muhimu sana kuhusiana na maombi.
   - Anasema nini kuhusu maombi katika mistari hii, na ni kwa namna gani anachokisema kinasaidia kutupa uelewa mzuri, na mpana zaidi kuhus maombi?
   - Sababu ya kuomba kitu mbele za Mungu ina nafasi gani kwake? Nia yetu inasema nini kuhusu sisi na hali yetu ya kiroho ndani?
   - Mistari hii inahusianaje na kile ambacho ni "injili ya mafanikio"?

3. Yak 4:4 ni moja kati ya mistari ya Biblia ambayo iko wazi sana iko bayana.
   - Kwa nini?
   - Ikiwa Wakristo binafsi na makanisa watatilia maanani mst. 4, unafikiri ni mabadiliko gani ambayo wengi wetu tutahitajika kuyafanya kibinafsi na kikanisa? Ni hatua gani tutachukuwa ili kufanya mabadiliko hayo?

[9] Katika nusu ya pili ya Ufunuo tunaona hii hali ya kuwa na pande mbili ikionyeshwa kupitia mifano inayokinzana inayohusu wanyama, wanawake, na miji: Mnyama—Mwana kondoo; Kahaba—Bwana arusi; Babeli mkuu—Yerusalemu Mpya.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

**VIII. <u>Yak 4:5-10—Jinsi ya kuitafuta neema ya Mungu na kupata hekima kutoka juu</u>—[5] *Au mwadhani ya kwamba maandiko yasema bure? "Huyo Roho akaaye ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu"? [6] Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, "MUNGU HUWAPINGA WAJIKUZAO, BALI HUWAPA NEEMA WANYENYEKEVU." [7]Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. [8] Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. [9] Huzunikeni na kuomboleza na kulia. Kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa hamu. [10] Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza.***

Aya hizi hutoa mshirika na dawa dhidi ya ubinafsi na matatizo yote ya kimahusiano ambayo huyasababisha ambayo yalijadiliwa katika **mst.1-4**. Hatimaye, jawabu hupatikana katika kujinyenyekesha kwa mtu na kumkaribia Mungu ambaye hutoa neema kwa wingi kwetu na kwa njia hiyo hutuinua. Mistari hii huibua maswala machache muhimu:

1. **<u>mst.5</u>**<u>—Swala kubwa la tafsiri.</u> Tafsiri ya hapo juu huchukua "Huyo" (ina maana, Mungu) kama mhusika mkuu wa mstari. Akiendeleza kile ambacho kimetangulia kusemwa katika **mst.4**—sura ya Mungu kama Bwana arusi wetu—mstari huu "unaelezea umuhimu wa kutochezacheza kwa namna yoyote na dunia kwa kuuzingatia ule wivu wa Bwana, ambao hudai utii mkamilifu usio na shaka wala kificho kutoka kwa wale watu ambao kwao amejiunganisha nao yeye mwenyewe" (Moo 1985: 144). Haiko wazi kwamba yule "roho" anamaanisha Roho Mtakatifu au kinyume chake "roho" yule ambaye alipuliziwa wakati wa uumbaji. Vyovyote iwavyo, mstari huu unatukumbusha sisi ya kwamba "Mungu anacho cha kudai kwetu kwa mujibu wa kazi yake njema aliyoitenda katika maisha yetu" (Ibid.: 146). Kwa upande mwingine, tafsiri ya Biblia ya NENO inasema, *"Au mwadhani kwamba Andiko lasema bure kuwa, huyo Roho ambaye Mungu amemweka ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu?"* Tafsiri hii huchukua "roho" kama mtendaji wa mstari (ina maanisha, yule "roho" aliyepulizia pumzi ndani ya mwanadamu wakati wa uumbaji) na hiyo humaanisha kwamba "kwa sababu ya asili yetu ya anguko, tuna namna ya kuwa na wivu" (*Life Application* 1986: 2250n.4.5). Bila kujali tafsiri, Yakobo hanukuu mstari fulani maalum au kifungu—anahitimisha fundisho la Maandiko." (*Life Application* 1986: 2250n.4.5).
2. **<u>mst.6</u>**<u>—Mungu hutupa sisi neema ya kutenda kulingana na vile anavyotaka na kushinda mwelekeo wa dhambi.</u> Mstari huu unanukuu **Mith 3:34** (angalia pia **1 Pet 5:5**). Ili uweze kuiishi hii neema, *unyenyekevu* unahitajika. Mistari wa **7-10** inayofuata inatueleza jinsi ya kuitumia nguvu ya Mungu katika maisha yetu.
3. **<u>mst.7-10</u>**<u>—Jinsi ya kujitwalia "neema kuu" ya Mungu.</u> Mistari hii minne inahusisha pia mambo kumi muhimu yanayoamriwa (amri) ambayo hupendekeza hatua saba ambazo twapaswa kuchukua ili tuielewe "neema kuu" ya mungu katika maisha yetu. Kama vile ambavyo "tunda la Roho" katika **Gal 5:22-23** yote huzungumzia namna "upendo" (ambao ni wa kwanza katika ile orodha ya tunda la roho) ulivyo, na sifa mbali mbali za kuwa kiongozi wa kanisa zilizoorodheshwa katika **1 Tim 3:2-7** yote huzungumzia ya kuwa "asiyelaumika" (ambayo ni ya kwanza katika orodha ya zile sifa) yukoje, kwa hiyo kilicho muhimu hapa kinaweza kuonekana kama kuelezea utii wa kweli kwa Mungu ukoje.
   - *Mtiini Mungu.* Hili ni jambo la msingi. Mambo yote yanayofuata hutiririka katika kumtii Mungu na huelezea kile kinachotakiwa ili uweze kumtii Mungu.
   - *Mpingeni Shetani.* Katika **mst.4**, Yakobo alionyesha kwamba kuna kutofautiana kukubwa sana kati ya Mungu na dunia. Sasa anadhihirisha kwamba mgogoro halisi uko kwa shetani. Sababu ni kwamba shetani ni *"mkuu wa ulimwengu huu"* (**Yohana 12:31**) na *"mungu wa dunia hii [au 'kizazi hiki']"* (**2 Kor 4:4**).
   - *Mkaribieni Mungu.* Hili ni mwenza wa kumpinga shetani. Kwa kuwa Shetani ni mtawala na mungu wa dunia hii, ye yote ambaye si sehemu ya ufalme wa Mungu yuko chini ya nguvu na mamlaka ya shetani (**Matendo 26:18**). Hakuna kuwa asiyefungamana na upande wowote au chaguo la tatu. Kwa kuongezea, David Nystrom anaelekeza kwamba kumkaribia Mungu "ni zaidi ya ile hali ya mtu kuamua kwamba anataka kuinua hali yake ya kiroho. Ni kuingia uweponi mwa Mungu kikamilifu, kukaa hapo, kujisikia vizuri hapo, kuwa nyumbani." (Nystrom 1997: 231)
   - *Itakaseni mikono yenu.* Mikono yetu humaanisha matendo yetu ya nje. Hata hivyo, hali hii lazima ifuatane na hatua ifuatayo.
   - *Safisheni mioyo yenu.* Mioyo yetu humaanisha mawazo yetu ya ndani, mwenendo, na nia. Ndivyo hasa visababisho vya asili vya matendo yetu ya nje. Yesu aliwaita wale amabao walisafisha mikono yao tu "makaburi yaliyopakwa chokaa" (**Math 23:27-28**; angalia pia **Luka 11:37-41**).
   - *Huzunikeni na kuomboleza na kulia; kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza.* Hili

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

linahusiana na ile hali ya kujuta hasa na kutubu dhambi zetu. Kristo amewaahidi kuwapa faraja wale wote watakaofanya hivyo (**Math 5:4**). Kwa upande mwingine, anatangaza ole kwa wale wanaocheka sasa kwa kuwa wataombeleza na kulia (**Luka 6:25**).

- *Jidhilini wenyewe.* Mwenendo wa unyenyekevu hudhihirisha kwamba tunamtii Mungu na tunamkaribia. Kwa kweli, mtu hawezi kumtii Mungu au kumkaribia kwa namna yoyote ispokuwa katika hali ya unyeyneykevu. Mungu atawainua wale wanaojinyenyekesha mbele zake, na kama Yakobo alivyosema katika **mst.6**, Mungu atauzawadia unyenyekevu wetu kwa kutupatia zaidi ya ile neema tunayoihitaji.

## MASWALI YA KUJADILI

1. Kwa kuwa Mungu "anawapinga wenye kiburi bali huwapa neema wanyenyekevu" (Yak 4:6), kuwa "mnyenyekevu" humaanisha nini, na tunawezaje kuwa wanyenyekevu?

2. Yak 4:7-10 inatupa maagizo kumi ambayo hupendekeza hatua saba za kutupatia "neema kubwa" ya Mungu katika maisha yetu.
   - Ni yepi hayo?
   - Ni kwa namna gani makanisa yanaweza kuwa saidia watu wao kuhusiana na hayo yaliyoagizwa katika mistari hii?

## IX. Yak 4:11-5:6—Dhambi ya kujitawala na madhihirisho yake ya nje

Kwa kuiangalia **4:7-10** ambayo huelezea kile ambacho tunapaswa kufanya na kile ambacho utii wa kweli kwa Mungu unahusisha, sehemu hii hutuonyesha kile ambacho *hatupaswi* kufanya, inamaanisha, ni ishara ambazo huonyesha kwamba mtu *hajajinyenyekesha* au hamtii Mungu.

**4:11-12—*[11] Ndugu, msisingiziane; amsingiziaye ndugu yake; au kumhukumu ndugu yake, huisingizia sheria na kuihukumu sheria. Lakini ukiihukumu sheria, huwi mtenda sheria, bali umekuwa hakimu. [12] Mtoa sheria na mwenye kuhukumu ni mmoja tu, ndiye awezaye huokoa na kuangamiza. U nani wewe umhukumuye mtu mwingine?***

Kumsingizia au kumhukumu ndugu ni ishara ya kiburi na ubinafsi. Ni kinyume cha mwenendo ambao tumeuona katika **4:5-10** ya kwamba tunapaswa kuwa nao. Neno la Kiyunani lililotumika hapa badala ya "kusingizia" (*katalaleō*) "husimama badala ya kila neno la kumsema mtu vibaya. Kile kinachosemwa kinaweza kuwa cha kweli katika yale yaliyomo lakini unakisema kwa namna ya ukali isiyopendeza na kwa chuki. . . . Yakobo anaponda kila haki ambayo wasomaji wake wanaweza kuwa nayo ya kudai kuhukumu juu ya jirani zake. Hii haimaanishi kwamba mahakama za kiserikali na mahakimu wake hawaruhusiwi. Badala yake, ni kuondoa ule ukali, chuki, roho ya ukosoaji ambayo siku zote hutafuta makosa ya wengine." (Burdick 1981: 196)

Swala hili ni zito sana kuliko watu wengi wanavyofikiri. Kama Ronald Ward anavyoonyesha, Yakobo anasema kwamba mtu mwenye roho ya kukosoa na kuhukumu namna hii na katika roho hiyo hunena kinyume cha wengine "amejifanya yeye mwenyewe kuwa *hakimu*; na si *hakimu* tu ambaye husimamia mambo ya sheria bali ni zaidi ya hapo. Amejifanya yeye mwenyewe kuwa ni *mtoa sheria.* Anakuwa tayari ametunga sheria nyingine ambapo kwa sheria hiyo yake anamhukumu ndugu yake. Jambo hili humkataa Mungu, humtenda dhambi Mungu na kwa kiburi huchukua nafasi yake Mungu." (Ward 1970: 1233)

Katazo la kuwahukumu wengine hapa halipingani na **Yohana 7:24** ambapo Yesu alisema, *"Basi msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki,"* au **1 Kor 2:15** ambayo inasema, *"Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu,"* au **1 Kor 14:29** ambayo inasema kusanyiko "*lipambanue"* kuhusiana na watu wanaodai kuwa wao ni manabii. Kila mmoja lazima aweze kutathmini na kupambanua tofauti iliyopo kati ya kweli na uwongo, zuri na baya, lililo sahihi na lisilo sahihi. Hayo ndiyo Yesu na Paulo waliyokuwa wakisema. Tofauti iliyopo kati ya kile alichokuwa akisema Yesu na Paulo na kile ambacho Yakobo anakisema hutuleta kwenye nia ya mtu, kuwa na nia na tabia ya Kristo, na kuongozwa na Roho. Dachollom Datiri anatamatisha hili katika maoni yake katika **1 Kor 2:14-15**: "Paulo anatofautisha kati ya aina mbili za watu. Aina ya kwanza ni wale ambao *hawana Roho*, ambao huishi kana kwamba hakuna kitu zaidi ya maisha ya mwili (**2:14**). Maisha yao huyathamanisha kwa vitu vya mwilini, na hutathmini kila kitu kwa thamani ya nje na mtazamo wao ni wa vitu. Watu wa jinsi hii hawaelewi, na hawawezi kuelewa mambo ya rohoni. Kinyume chake, wale ambao wamekomaa au watu wa rohoni hutawaliwa na Roho,

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

wanaifurahia ile fursa ya *kuyatambua yote*, maana yake ni kwamba, wanaweza kuchunguza kwa makini na kuchuja kile cha muhimu (**2:15**). Mtu yule mwenye nia ya Kristo ana uwezo wa kufanya maamuzi sahihi kuhusiana mambo." (Datiri 2006: 1381)

***4:13-17***—*[13] **Haya basi, ninyi msemao, "Leo au kesho tutaingia katika mji fulani na kukaa humo mwaka mzima, na kufanya biashara na kupata faida;" [14] Walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka. [15] Badala ya kusema, "Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi." [16] Lakini sasa mwajisifu katika majivuno yenu; kujisifu kote kwa namna hii ni kubaya. [17] Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.***

Wakati ambapo **mst.11-12** ilihusisha kusingizia na kuhumu wengine, katika mistari hii dhambi ya msingi inayokabiliwa hapa ni *mwenendo wa ndani* wa maisha: mwendo wa kujitawala au hali ile ya mtu kujiona anajitosheleza, maana yake ni, mtu kuishi maisha yake bila ya kumtaja Mungu. Inahusiana kabisa na ile dhambi ya kiburi, ina maana, kudhania kwamba mipango yako yote unayopanga bila ya Bwana, itakwenda kama ulivyopanga pasipo kuelewa kwamba Mungu yuko juu ya vitu vyote na anaweza kuwa na mipango mingine tofauti. Kiburi cha jinsi hiyo ni majivuno, kama Yakobo anavyobainisha katika **mst.16**.

Kuwa na mipango kwa ajili ya wakati ujao silo jambo linalohukumiwa hapa kama ambavyo kupambanua, kutathmini na kuhukumu, *peke yake*, vilihukumiwa katika **mst.11-12**. Kila mmoja kwa kadiri ya uhitaji wake yampasa apange mambo yake ya wakati ujao. Lakini mipango yetu yote lazima ipangwe katika muktadha wa kuwepo kwa Mungu, mapenzi yake, na mipango yake. Lazima wakati wote tuweke katika ufahamu wetu kwamba mipango yetu si ya hakika sana juu ya mapenzi yake na mipango yake. Katika nyakati mbali mbali, Paulo kwa imani alikabidhi mipango yake kwa maneno kama "Mungu akinijalia" (angalia **Matendo 18:21; Rum 1:10; 1 Kor 4:19; 16:7**; angalia pia **Ebr 6:3**). Hakufanya hivyo kila wakati alipokuwa akipanga kitu (angalia **Matendo 19:21; Rum 15:28; 1 Kor 16:5, 8**). Hili litukumbushe kwamba kusema maneno kama "Mungu akipenda" sio "maneno ya kichawi" ambayo yanaweza kutatua tatizo lako. Badala yake, swala hili liko katika mwenendo wetu wa ndani: ikiwa kwa imani ya dhati tunasema maneno kama "Bwana akinijalia" au la, "kwa kudhamiria ndani yetu tunaweka mipango yetu yote na matumaini chini ya Ubwana wa Kristo, tukitambua kwamba yeye ndiye anayefanikisha au kusababisha mipango hiyo ilete huzuni" (Moo 1989: 1160). Yakobo ahanahitimisha sehemu hii katika **mst.17** kwa kutuonyesha kwamba kwa kuwa sasa tunajua mwenendo sahihi ambao tunapaswa kuwa nao kuhusiana na mipango yetu, kushindwa kuweka mipango yetu chini ya mapenzi na mipango ya Mungu ni dhambi. Kwa upande mwingine, ikiwa tutaamini kiukweli, tukapokea na kukaa katika kweli ya ukuu wa Mungu na kutegemea yeye kikamilifu yale mapenzi yake (angali, mfano, **Yohana 15:5; 1 Kor 6:19-20**) tunaweza kuwa na amani tele kama mipango yetu itafanikia au la.

***5:1-6—Haya basi, enyi matajiri! Lieni, mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia. [2] Mali zenu zimeoza, na mavazi yenu yameliwa na nondo. [3] Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto. Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho. [4] Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi. [5] Mmefanya anasa katika dunia, na kujifurahisha kwa tamaa; mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo. [6] Mmehukumu mwenye haki mkamwua; wala hashindani nanyi.***

Sehemu hii inafuatia kutoka **4:13-17** kuhusiana na asili ya kupita ya maisha na kutokuwa na mipango ya kibinafsi kwa kiburi na pia maoni ya ziada katika **1:9-11**. Mada ya maonyo dhidi ya matajiri inajulikana katika mafundisho ya Yesu (angalia **Math 6:19-24; 19:23-24; Marko 10:23-25; Luka 12:16-21; 16:19-31**) na Paulo (**1 Tim 6:5-11**).

Katika kifungu hiki Yakobo anatumia lugha ile ile ambayo Yesu aliitumia kuhusiana na matumizi ya pesa ili kuwahukumu matajiri. Yesu alisema, *"Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; [21] kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwepo na moyo wako."* (**Math 6:19-20**) Yakobo anasema kwamba matajiri *wameweka* "hazina zao duniani." Mtu huwa anajiwekea hazina yake duniani kwa kupenda pesa na vitu, kwa kuwa tamaa inayoendelea na kujibidiisha sana kutengeneza na kuwa na pesa zaidi, kwa kuhodhi pesa zake na kuzitumia kwa matumizi ya kibinafsi badala ya kutoa kwa ukarimu kuwasaidia maskini na wahitaji, na kwa kuishi maisha ya anasa iliyozidi sana na uasherati. Mbele ya macho ya Mungu, utajiri wetu "huoza" na "kupata kutu" na mavazi yetu "huliwa na nondo" tunapokusanya mali kwa ajili ya "ubinafsi" badala ya kutumia katika kuwasaidia wengine na kuueneza ufalme wa Mungu (angalia **1 Tim 6:17-**

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

**19**).

Vipengele vingine vitatu katika sehemu hii inabidi vitajwe. Kwanza, katika **mst.4** vilio vyao wavunaji ambao wamefanya kazi katika mashamba ya matajiri lakini hawakulipwa ipasavyo *"vimefika masikioni mwa Bwana wa Majeshi."* Hii inarudia maneno ya **Mwz 4:10** wakati damu ya Habili ilipolia kutoka katika ardhi hadi kwa Bwana. Si tu vilio vya watendakazi ambavyo vinamfikia Bwana, lakini *"ujira wa wakulima . . . unalia dhidi yenu."* Hili linafanana na **mst.3** ambao unasema *kutu* ya dhahabu na fedha za watu matajiri yenyewe *"itakuwa shahidi dhidi yao."* Zaidi ya hapo, Mungu anaitwa "*Bwana wa majeshi*" (wakati mwingine ikitafsiriwa *"Bwana wa Majeshi"*). "Majeshi" humaanisha majeshi na hutilia mkazo ile sifa ya Mungu kuwa mwenye nguvu zote (Danker 2000: *Majeshi,"* 909; Zodhiates 1993: *"Majeshi,"* 1268). Hili huonyesha kwamba Mungu anaingia vitani dhidi ya matajiri kwa niaba ya maskini ambao wamewatenda vibaya. Mahali pengine katika AJ ambapo Mungu anaitwa Bwana wa Majeshi ni katika **Rum 9:29**, ambapo pia huzungumzia kuhusu Sodoma na Gomora. Jambo hili ni muhimu kwa kawa ni kwa ajili ya dhambi zile zile ambazo Yakobo anazitaja hapa—kupenda pesa na vitu, kulimbikiza na kutumia pesa kwa ubinafsi badala ya kutoa kwa ukarimu ili kuwasaidia maskini na wahitaji, na kuishi maisha ya anasa, ya kutapanya ya kiasherati—kiasi kwamba Mungu akaiharibu Sodoma na Gomora (**Ezek 16:49-50**).

Pili, **mst.3** unasema, *"Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho!"* Watu wengine hufikiri kwamba "siku za mwisho" ni wakati fulani ujao ambao utakuwa kabla Yesu hajarudi mara ya pili. Hiyo si kweli. Kuja kwa Kristo mara ya kwanza: (A) ni ishara ya mwanzo wa "siku za mwisho" ambayo itaendelee mpaka kurudi kwake; na (B) kulitimiza nabii za AK kuhusiana na "siku za baadaye" au "siku za mwisho." AJ huliweka jambo hili wazi. "Hili limetamkwa bayana na Petro katika hotuba yake kuu siku ile ya Pentekoste, alipokuwa akinukuu kutoka katika unabii wa Yoeli kama ifuatavyo: 'Kwa kuwa watu hawa hawakulewa, kama mnavyodhani, kwa maana ni saa tatu ya mchana, lakin jambo hili ni lile lililonenwa na kinywa cha nabii Yoeli: Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu . . .'" (Matendo 2:16-17). Maneno 'itakuwa siku za mwisho' (*en tais eschatais hēmerais*) ni tafsiri ya maneno ya Kiebrania *'acharey khēn,* maneno halisi humaanisha *baadaye.* Wakati Petro aliponukuu maneno haya na kuyatumia katika lile tukio ambalo lililokuwa ndio anasema: 'Tuko katika siku za mwisho sasa.'" (Hoekema 1979: 16) Kila wakati msemo "siku za mwisho" unapotumika katika AJ basi hapo inamaanisha kwamba tuko katika "siku za mwisho" sasa (angalia **2 Tim 3:1-5; Ebr 1:1-2; 2 Pet 3:1-4**). Kwa hivyo, Yakobo anazungumzia kuhusu watu na kile wanachofanya na pesa zao *sasa*.

Tatu, muktadha wa kifungu chote ni kwamba mali za watu matajiri hapa ni ishara, si ya *upendeleo* wa Mungu bali ya *hukumu* yake. Watu wengi wanafikiri kwamba utajiri ni ishara ya upendeleo wa Mungu. Ni kweli bila shaka, Mungu *"hutupatia kwa wingi vitu vyote ili tuvifurahie"* (**1 Tim 5:17**). Lakini fundisho la "injili ya mafanikio" ya kwamba utajiri ni ishara ya upendeleo wa Mungu ni uongo ulio wazi. Yesu alikuwa mtu maskini ambaye aliteswa na watu tajiri na wenye nguvu, hatimaye alikamatwa, akapigwa, akashtakiwa kwa uongo na kusulibiwa kama mhalifu wa kawaida au mtumwa. Paulo alikuwa tajiri lakini hapo ni *kabla* ya kuwa Mkristo. *Baada* ya kuwa Mkristo alipigwa kwa mijeledi na mawe, aliharibikiwa merikebu, aliteswa, alifungwa (**2 Kor 11:23-33**) na mwishowe kichwa chake kilikatwa. Mambo hayo yote yaliyotukia kwa Yesu na Paulo yaliwapata si kwa sababu hawakuwa na imani au walitenda dhambi; mambo hayo yalitukia kwao hasa *kwa sababu* walikuwa waaminifu. Ishara inayoonyesha kwamba sisi tu wanafunzi wa Yesu si kule kuwa na pesa au afya bali wakati tunapokuwa tunapendana sisi kwa sisi (**Yohana 13:34-35**).

Mali *zinaweza kuwa* ishara ya Baraka za Mungu na upendeleo wake—lakini hilo hutegemea sana na kile tunachikifanya kwa kutumia kile ambacho Mungu ametubariki kwacho. Wazo la Yakobo ni kwamba, ikiwa tunalimbikiza pesa zetu na kuzitumia kwa ajili yetu wenyewe, kuishi maisha ya anasa na starehe badala ya kutumia kile ambacho Mungu katubariki kwacho kuwasaidia maskini na wahitaji na kueneza ufalme wa Mungu, utajiri wetu ni ishara ya *hukumu* ya Mungu*!* Anaweka hili wazi katika **mst.3** ambao unasema, *"Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto"* na katika **mst.5** ambao unasema, *"Mmefanya anasa katika dunia, na kujifurahisha kwa tamaa; mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo."* Katika **mst.5** analinganisha matajiri na ng'ombe na nguruwe ambao hunenenpeshwa ili wachinjwe. Ile *"siku ya kuchinjwa"* ni neno la AK linalomaanisha siku ya hukumu (**Yer 12:1-3**; angalia pia **Zab 49:20**). Yakobo anatuhabarisha sisi kwamba, kama wanyama ambao wako katika maandalizi ya kuchinjwa, matajiri, katika utajiri wao na raha, hawana habari—hata siku ile ya kifo chao—ya kwamba wako karibu na hukumu na kuchinjwa. Na, kama **mst.3** unavyotuonyesha, ule utajiri wao wenyewe (ambao ndio wameutegemea na ambao waliufikiria kwamba ni ishara ya upendeleo wa Mungu) utakuwa shahidi *dhidi* yao siku ile ya hukumu. Ni ushahidi dhidi yako kwa sababu waliutumia kwa ajili yao wenyewe badala ya kuutumia kwa kuwasaidia wengine na kueneza ufalme wa Mungu.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Kutajwa kwa kuuliwa kwa mtu mwenye haki katika **mst.6** “kunaweza kumaanisha yale matokeo ya kule kushindwa kwa tajiri kutumia mali zake na wenye uhitaji na kuwalipa wafanyakazi ujira wao. . . . Hata hivyo, *hukumu* (*katadikazō*) ni neno la kimahakama, na hudokeza kwamba badala ya kwamba matajiri wanatumia, pengine hupotosha, taratibu za kisheria zilizopo ili waweze kujikusanyia vitu na mali.” (Moo 1985: 166) Kifungu cha manenno cha mwisho, *“wala hashindani nanyi,”* kwa ujumla kinamaanisha kwamba matendo ya matajiri ni mabaya kwa sababu wahanga wao hukataa au hawana uwezo wa kukataa. Hata hivyo, “haiwezekani kukitafsiri kifungu kama swali, ukitarajia jibu la ‘ndiyo’: ‘Je hashindani?’ Mtenda wa tendo hapo angekuwa Mungu . . . na kinachozungumziwa hapo kingekuwa ni hukumu ijayo: ‘je Mungu hatasimama kinyume chenu ninyi?’” (Ibid.: 167)

Katika sehemu hii, Yakobo anatuambia sisi kwamba, mwisho wa yote, pesa ni za kiroho. Kile tunachofanya na pesa zetu, pengine kuliko kitu kingine cho chote, hudhihirisha ni nani Bwana wetu hasa. Ndiyo maana Yesu alisema zaidi ya mara moja, *“Hamwezi kumtumikia Mungu na mali”* (**Math 6:24; Luka 16:13**).

## <u>MASWALI YA KUJADILI</u>

1. Yak 4:11-12 inazungumza kuhusu kusema kinyume na ndugu na kumhukumu.
   - Ni nini kinachofanya jambo hili kuwa dhambi mbaya?
   - Je, hili linatofautiana na Yesu aliyesema, “Hukumu kwa hukumu iliyo ya haki” (Yahana 7:24; angalia pia 1 Kor 2:15 na 1 Kor 14:29)? Unamfananishaje Yakobo na Yesu na Paulo?

2. Yak 4:13-17 inazungumzia kuhusu kuishi maisha yako kwa mwenendo wa kijitawala au kujitosheleza bila ya kumtaja Mungu. Tunawezaje kuishinda tabia hii (ambayo kila mmoja anayo kwa kiwango kimoja au kingine) na kwa makusudi tuiweke mipango yetu kwenye mpango na mapenzi ya Mungu?

3. Yak 5:1-6 ni onyo kali sana dhidi ya matajiri na walafi.
   - Hakuna anayeamini kwamba yeye ni mlafi, lakini tunawezaje kujua kama sisi tu walafi kweli au la?
   - Katika kifungu hiki, utajiri wa mtu ulikuwa ndiyo ishara , sio ya upendeleo wa Mungu kwa huyo mtu, bali hukumu ya Mungu dhidi yake (ni kipi “kitashuhudia dhidi yako”). Kila mmoja anahitaji pesa na vitu, lakini tutajuaje kama utajiri ambao tumeuchuma ni ishara ya Baraka za Mungu au hukumu yake?
   - Yakobo anasema kwamba watu hawa wameweka akiba utajiri wao kwa ajili ya “siku za mwisho.” “Siku za mwisho” ni lini, na tutajuaje?
   - Kusema pesa ni ya kiroho humaanisha nini?
   - Kanisa linaweza au linapaswa kufanya nini ili kuwafundisha watu wake kuhusiana na asili ya kiroho ya pesa na jinsi ambavyo watu wanapaswa kutawala pesa zao inavyofaa?

## X. <u>Yak 5:7-20—Nasaha za kuhitimisha</u>

**<u>5:7-11</u>—*[7] Kwa hiyo ndugu, vumilieni, hata kuja kwake Bwana, Tazama, mkulima hungoja mazao ya nchi yaliyo ya thamani, huvumilia kwa ajili yake hata yatakapopata mvua ya kwanza na ya mwisho. [8] Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia. [9] Ndugu, msinung’unike, msije mkahukumiwa. Angalieni, mwamuzi amesimama mbele ya mlango. [10] Ndugu, watwaeni manabii walionena kwa jina la Bwana, wawe mfano wa kustahimili mabaya, na wa uvumilivu. [11] Angalieni, twawaita heri wao waliosubiri. Mmesikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma.***

“Kwa hiyo,” maneno yanayoanzisha sehemu hii, huunganisha **mst.1-6** na kuja kwa Kristo mara ya pili na hivyo huwekea mkazo ile mada ya hukumu katika mistari hiyo.[10] Kwa hakika, ile rai ya kuwa tuvumilie (**mst.7-8**), tusinung’unikiane (**mst.9**), kustahimili mabaya (**mst.10-11**), kuzungumza kwa kawaidi na kwa kweli (**mst.12**), kuomba, kuimba sifa, na kuungama dhambi (**mst.13-18**), na kumrejeza kwa Bwana ndugu aliyepotea (**mst.19-20**) hizi zote zinaweza kuonekana kuwa ni nasaha za namna ya kuishi tukiwa tunajua kwamba Yesu anarudi tena. **Zaburi 37** ina mtazamo unaofanana kuhusiana na usalama wa wale wanaofanya mambo sahihi na kuishi kwa ajili ya Bwana dhidi ya kutokuwa salama na hukumu ijayo kwa wale ambao hawafanyi yaliyo sahihi (angalia pia **Zaburi 73**).

---

[10] “Bwana” katika **mst.7** ni sawa kama “Bwana wa majeshi [Bwana wa Majeshi]” katika **mst.4**. “Bwana” katika **mst.7** kwa wazi inazungumzia kule kuja kwa Kristo mara ya pili; “Bwana wa majeshi” katika **mst.4** ni maelezo ya AK kumhusu Mungu. Kwa hivyo, Kristo ni Mungu.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Utofauti wa jinsi Mkristo anavyopaswa kuishi ikilinganishwa na yale ambayo Yakobo ameyajadili katika **mst.1-6** unaonekana pia katika utofauti kati ya matajiri ambao *"wamejilisha mioyo yao"* (**mst.5**) dhidi ya waaminio ambao wanapaswa *"kuthibitishwa mioyo yao"* (**mst.8**). Dhamira ya uvumilivu ambayo inaaza sehemu hii inatumika katika vipendele vyote mahususi anavyovijadili Yakobo: kushindwa kuvumilia husababisha kunung'unika (**mst.9**); na kustahimili mabaya (**mst.10-11**) huhitaji uvumilivu. David Nystrom anaonyesha sababu moja muhimu kwa nini Yakobo anawaita waaminio kuvumilia mabaya kwa saburi: "Faida mojawapo itokanayo na kuvumilia mateso ni kwamba tunapata fursa ya kuwahudumia wengine ambao pia wako katika mateso. Haya ni maneno magumu, lakini ni kweli. Mke wangu na mimi tumeoana kwa miaka kumi na tano na hatuna watoto. Daktari anasema kwamba hatutaweza kupata watoto kamwe. Huzuni na hisia zisizotarajiwa za hitaji hili linaloumiza ni ngumu kuzieleze. Lakini mimi na mke wangu tumeweza kwenda sambamba na wengine ambao wana maumivu kama yetu—maumivu ya mama ambaye mtoto wake amekufa wakati wa kuzaliwa, au yale ya wanandoa ambao, kama sisi, hawana watoto. Siwezi kusema ya kwamba tunafarijika sana kuwa katika hali hii, lakini tumegundua kwamba hii ni fursa ambayo tunaweza kuwa wa msaada." (Nystrom 1997: 297-98)

Kwa kuongezea, katika **mst.7**, **8**, na **9** uvumilivu unahusishwa na kuja kwa Bwana na hukumu atakayoileta. Ingawaje jukwaa la Mungu ni kubwa na wigo wa muda wake ni mkubwa kuliko vile ambavyo tungependa, *a*-nakuja tena, na hakuna ambacho kinasahauliwa au kutotazamwa. Haki *ita*-tendeka, na watakatifu wa*ta*pata thawabu. Lakini Mungu amefanya zaidi ya kutuhakikishia sisi ya kwamba atahukumu wanadamu kwa haki kwa sababu ya dhambi zao, makossa, na uovu; alibeba dhambi zetu na kulipa kima kwa ajili ya dhambi zetu ili kwamba wale wote wanamgeukia wapokee uzima badala ya mauti ya milelel siku ya hukumu. Kwa kuyajua haya yote, mwandishi Mkrisro wa Kirusi Fyodor Dostoevsky alihitimisha, "Ninaamini kama mtoto ya kwamba mateso yataponywa na kupatiwa utatuzi. Ninaamini kwamba mambo yote ya kipuuzi ya kuaibisha ya kuhitilafiana kwa wanadamu yatatoweka kama mazigazi, ni kama uzushi wa kudharaulika usio na nguvu wa ufahamu mdogo sana wa mwanadamu. Ninaamini kwamba wakati wa mwisho wa dunia, katika wakati wa amani ya milele, kitu fulani cha thamani sana kitatokea ambacho kitatosha kwa ajili ya mioyo yote, kwa ajili ya kufariji maumivu yote ya moyo, kwa ajili ya upatanisho wa makosa yote ya jinai ya wanadamu wote, kwa ajili ya damu yote iliyomwagwa. Ninaamini kwamba si tu kwamba itawezekana kusamehe lakini kuhesabia haki kila kilichotokea." (Dostoevsky 1957: 217) Kwa kuliweka hili sawa sawa katika ufahamu, Mkristo ataweza kuvumilia na kukabili cho chote ambacho anakutana nacho sasa.

**5:12—*Lakini zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, wala kwa mbingu wala kwa nchi; wala kwa kiapo kinginecho chote; bali ndiyo yenu na iwe ndiyo, na siyo yenu na iwe siyo, msije mkaangukia hukumu.***

Yakobo hapa anaoanisha na kile ambacho Yesu alisema katika **Math 5:33-37**. Kwa kuwa Yesu ni kweli (**Yohana 14:6**; angalia pia **Yohana 1:14**), Wakristo—zaidi ya watu wengine hapa duniani—wanapaswa kuwa watu wa kweli na uadilifu.

**5:13-18—*[13] Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi. [14] Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. [15] Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. [16] Ungameni dhambi zanu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii. [17] Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe, na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita. [18] Akaomba tena, mbingu zikatoa mvua, nayo nchi ikazaa matunda yake.***

Katika sehemu hii, **mst.13-16a** huzungumzia kuhusu maombi katika hali zote za maisha; **mst.16b-18** huzungumzia nguvu ya maombi ya kumaanisha. "Mateso" katika **mst.13a** huonyesha shida au matatizo ya aina yoyote—ya kimwili, kiroho, kiakili, kihisia, kifedha, kimahusiano nk. Vivyo hivyo, "kuchangamka" katika **mst.13b** "haihusu hali ya matukio ya nje, lakini uchangamfu na furaha ya moyoni ambayo mtu anakuwa nayo awe katika wakati mzuri au mbaya. . . . mioyo yetu inapokuwa imefarijiwa, ni rahisi kabisa kusahau kwamba utoshelevu huu mwishoni mwa yote unatoka kwa Mungu. Hivyo, pengine hata zaidi ya wakati wa mateso, ni lazima tukumbushwe katika nyakati za furaha kuhusu wajibu wetu wa furaha wa kukubali nafasi kuu ya Mungu katika maisha yetu. Tunapaswa kufanya hili, Yakobo anasema *kuimba zaburi*. . . . huku kuimba zaburi kulikuwa na uhusiana wa karibu na maombi (*cf.* 1 Kor. 14:15); hakika, inaweza kuchukuliwa kama aina ya maombi." (Moo 1985: 175-76)

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Kuna vipengele kadha wa kadha vya kuwaombea wagonjwa katika **mst.14-16a** ambavyo vinapaswa kuangaliwa. Kwanza, maneno yaliyotumika katika mistari hii—"hawezi" (**mst.14**); "kumpaka mafuta" (**mst.14**); "kutamwokoa" (**mst.15**); "atamwinua" (**mst.15**); na "kuponywa" (**mst.16a**) wakati mwingine yanatumika katika Biblia katika muktadha wa kiroho ukihusisha wokovu, badala ya ugonjwa wa mwilini na uponyaji wa mwilini.[11] Hata hivyo, muktadha hapa unaonekana kuwa ni wa ugonjwa wa mwilini na uponyaji wa mwilini (Moo 1985: 181).

Pili, "wazee" ambao walikuwa waombe na kumpaka mgonjwa mafuta walikuwa ni viongozi wa kiroho wa makanisa ya mahali pamoja (angalia **Matendo 14:23; 20:17; 1 Tim 5:17; Tito 1:5; 1 Pet 5:1**). "Kupaka mafuta" ni jambo ambalo lilionekana lina matokeo ya kitabibu katika nyakati za Biblia (angali **Luka 10:34**), jambo ambalo limewafanya baadhi ya wafafanuzi kuhitimisha kwamba "Yakobo anatumia maombi na dawa ili kutibu" (Burdick 1981: 204). Hata hivyo, wengi wao na pengine mtazamo ulio mzuri unaona kule kupaka mafuta kuwa ni tendo la ishara kwamba yule mgonjwa anatengwa kwa ajili ya kuhudumiwa kimaalum na Mungu (angalia Moo 1985: 179; Moo 1989: 1162). Hili linaonekana katika ukweli kwamba kule kupaka mafuta inabidi kufanyike *"katika jina la Bwana"* (**mst.14**), na kupaka mafuta ni ishara ya utendaji au uwepo wa Roho Mtakatifu (angalia **1 Sam 16:13; Zab 89:20; Luka 4:18; Matendo 10:38**). Kuna tahadhari mbili zinazohusiana ambazo ni lazima kuzingatiwa katika fahamu zetu kuhusiana na matumizi ya mafuta ya upako:

- "Maombi ndilo jambo muhimu kati ya hizi huduma mbili zinazofanywa na wazee. "Omba" ndilo tendo kuu, wakati "paka mafuta" ni tendo linalofuata. Zaidi ya hayo, mkazo mkubwa wa kifungu chote ni maombi. Kwa hiyo kupaka mafuta ni tendo linalofuatia." (Burdick 1981: 203-04)
- "Kinachoponya sio yale mafuta wala wale wazee, lakini ni Bwana mwenyewe, kwa kuwa upakaji wa mafuta unafanywa kwa jina lake. Wengine katika Afrika huamini kwamba ni yale mafuta hasa ambayo yana nguvu ya kimiujiza ya kuponya. Wengine hufikiri kwa swala la kupona linategemea hali ya ubora ya yale mafuta yanayotumika. Watu wa jinsi hiyo lazima waache kufikiri juu ya mafuta kama kitu wakfu au kama yana nguvu maalumu na wang'ang'anie ahadi za Mungu tu. Ndiyo maana mwandishi wa waraka huu alipendekeza maombi (**5:15**). Ni maombi ya imani ndiyo yanayoleta uponyaji kimiujiza badala ya marudiorudio ya fomyula maalumu." (Andria 2006: 1516)

Tatu, yale "maombi ya imani" yanaunganishwa na msamaha wa dhambi katika **mst.15**. Kuna tahadhari tatu ambazo yabidi kuzingatiwa katika fahamu hapa:

- Ingawaje magonjwa mengine na kifo vinaweza kusababishwa na dhambi (**1 Kor 11:27-30**), Biblia inaweka wazi ya kwamba ugonjwa sio lazima uwe umesababishwa na dhambi (**Yohana 9:2-3**). Yakobo analikubali hilo mwishoni mwa **mst.15** anaposema *"<u>hata</u> ikiwa amefanya dhambi."*
- Kuunganishwa kwa uponyaji na msamaha katika **mst.15** (*"hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa"*) "kumewafanya wengine kufikiri kwamba uponyaji wa mwili ni kiungo muhimu cha wokovu. Tatizo lililopo katika kuamini hivyo ni kwamba mtu anaweza kuugua mara kwa mara na kuponywa kwa maombi. Lakini siku moja mtu yule anaweza kuugua na hatimaye akafa. Kifo cha jinsi hiyo hakimaanishi kuwa mtu yule amepoteza wokovu wake. Wokovu wetu ni wa hakika na wa milele. Kile ambacho kifungu hiki kinafundisha ni kwamba uponyaji wa mwili ni ishara ya ukombozi wetu." (Andria 2006: 1516) Ukweli ni kwamba watu wote, ni pamoja na Wakristo wote, wako kwa muda. Wakristo wengine wana matatizo fulani ya kiafya na hayaponi *kamwe*, licha ya maombi na imani kubwa (angalia, mfano, **2 Kor 12:7-10** ["mwiba katika mwili" wa Paulo]). Ukweli huu unatupeleka katika tahadhari ya tatu:
- Wakati **mst.15** unasema *"kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule,"* si maombi peke yake ambayo yana nguvu maalumu ya kuponya kuliko ile nguvu ya kuponya iliyomo katika mafuta ya upako—ni Mungu ndiye anayeponya. "Kwa hiyo, maombi ya kweli ya imani, wakati wote yanahusisha shukrani ya kimya kimya kuhusiana na ukuu wa Mungu katika mambo yote; ya kuwa ni mapenzi ya Mungu ndiyo ambayo lazima yafanyike. Na ni wazi kwamba kwa vyovyote vile wakati wote ni mapenzi ya Mungu kuwaponya wale wanaoumwa (*cf.* 2 Kor. 12:7-9). Kwa hiyo, ile 'imani' ambayo ni sharti la lazima ili maombi yetu ya kuponywa yajibiwe—imani hii inakuwa karama ya Mungu—inaweza kuwepo kiukweli wakati ule ambapo ni mapenzi ya Mungu kuponya. . . . Katika maisha haya, hatutaweza kujua, mara nyingi, ikiwa mapenzi ya Mungu ni kuponya; hatutaweza wakati wote kuhisi ikiwa ile 'imani' ambayo inapata kile kilichoombwa ipo. Wakati maombi yetu yanayotoka moyoni, na yenye nguvu, kwa ajili ya uponyaji

[11] Ronald Ward anahoji, "Utata unaosababishwa na maana tofauti za maneno haya hauwezi kupingwa. Inawezekana kutoa tafsiri yenye msimamo wa kitabibu au tafsiri yenye msimamo wa kiroho. Ama mtu ni mgonjwa na *maombi ya imani* yatamponya na *Bwana atamwinua* kutoka katika kitanda chake; au hajiwezi na amechoka kiroho na ataokolewa katika ufufuo wa kiroho. Yakobo anaweza kuwa ameamua kuwa mtata kwa makusudi, akiwaachia wasomaji wake kuchagua ile tafsiri ambayo inakubaliana na matokeo ya kuja kwa wazee." (Ward 1970: 1235)

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

yasipojibiwa, hapo basi, si upungufu wetu wa imani ambao umesababisha hilo; katika muktadha ambao imani ya jinsi hiyo ingekuwepo haikuwepo." (Moo 1985: 182, 186-87)

Nne, **mst.16a** unawasihi kusanyiko lote (sio tu wazee) *"ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpata kuponywa."* Wakristo wengi huombeana wao kwa wao, ingawaje bila shaka inafanyika mara chache au, angalau hapa na pale. Kwa upande mwingine, ni Wakristo wachache huungamiana dhambi hasa. Dietrich Bonhoeffer anajadili kwa nini hili ni muhimu sana: "Katika kuungama mtu hupenya kwenye hakika. Ni kwa nini mara nyingi ni rahisi kwetu kukiri dhambi zetu kwa Mungu kuliko kwa ndugu katika Bwana? . . . Ni lazima tujiulize kama hatujakuwa tukijidanganya wenyewe na maungamo yetu ya dhambi mara kwa mara kwa Mungu, kama badala yake hatujakuwa tukijiungamia dhambi sisi wenyewe na pia kujipatia wenyewe msamaha. Na je hii si sababu pengine ya kuona kwamba ile hali ya kurudiarudia maovu na ule udhaifu wa utii katika Ukristo wetu inatokana na ukweli kwamba tunaishi katika kujisamehe wenyewe na sio katika msamaha halisi? . . . Ni nani anaweza kutuhakikishia kwamba, katika kuungama na kusamahewa dhambi zetu, hatujikabili sisi wenyewe bali tunakabiliana na Mungu aliye hai? Mungu anatupa sisi uhakika huu kupitia ndugu katika imani. Ndugu katika imani huvunja ule mzunguko wa kujidanganya mwenyewe. Mtu anayekiri dhambi zake mbele ya ndugu yake kiimani anajua kwamba sasa hayuko peke yake; anauona uwepo wa Mungu katika uhalisia wa yule mtu mwingine. . . . Kama ambavyo ukiri wa wazi wa dhambi zangu kwa ndugu unanihakikishia usalama dhidi ya kujidanganya, vivyo hivyo uhakika wa msamaha unakuwa hakika zaidi unapotamkwa na ndugu wa imani kwa jina la Mungu. Mungu ametupa sisi kuungamiana sisi kwa sisi ili tuwe na uhakika na msamaha wa kiungu." (Bonhoeffer 1954: 115-17)

Mstari **16b-18** baada ya hapo unaendelea kujadili matokeo ya maombi. "mwenye haki" (**mst.16b**) si mwanachama wa "daraja" fulani maalumu la Wakristo (maaskofu, wazee, jamii ya makasisi, nk.) au yule ambaye ana karama fulani maalumu, lakini ni ye yote yule ambaye ana uhusiano mzuri na Mungu: mtu ambaye amezikiri dhambi zake na kusamehewa, ambaye anampenda Bwana, ambaye kwa makusudi anatafuta kumtii Mungu na anawapenda na kuwatumikia wengine. Mfano wa Eliya unakazia hili. Ingawaje Eliya alikuwa nabii mkuu, Yakobo anakazia kwamba *"Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi"* (**mst.17**). Kwa hakika, **1 Fal 19** inadhihirisha kwamba Eliya aliogopa (**1 Fal 19:3**); alipata mfadhaiko (**1 Fal 19:4**); na alijawa na hali ya kujihurumia (**1 Fal 19:10**). Pamoja na hayo yote, makabiliano ya Eliya na manabii wa Baali na matukio ambayo yalitokea baadaye (**1 Fal 18-19**) yanatupa ishara ni kwa nini maombi yake yaliweza kuleta matokeo makubwa: nguvu yake ilielekeza na ilitafuta kumtukuza Mungu badala ya kujitukuza yeye mwenyewe (**1 Fal 18:36-39**); alimtarajia Mungu kuleta matokeo (**1 Fal 18:41**); aling'ang'ania katika maombo (**1 Fal 18:42-45**); alitenda na aliwaita watu kutenda sawa sawa na Neno la Mungu na mapenzi yake (**1 Fal 18:40**); aliishi katika uhusiano wa karibu, na alikuwa na raghba na Bwana (**1 Fal 18:46; 19:9-14**); na alikuwa mtii kwa neno la Bwana (**1 Fal 19:5-8, 15-19**).

**5:19-20—**[19] ***Ndugu zangu, ikiwa mtu wa kwenu amepotelea mbali na kweli, mtu mwingine akamrejeza;*** [20] ***jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi kata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi.***

Mistari hii miwili inafunga waraka wa Yakobo kwa mkazo wa kimatendo ambao ndio umekuwa ujumbe wa waraka wote. Kuna utata hapa kama huyu ambaye amepotelea mbali na kweli ni mwamini wa kweli ambaye anarudi nyuma katika dhambi ingawa bado yu miongoni mwa waliokombolewa au ni mwenye kukiri Ukristo kwa uongo ambaye anahitaji wokovu. (Kanisa wakati wote limekuwa "kusanyiko la watu mchanganyiko" likiwa na watu ambao wameokoka na wengine ambao hudai kuwa wameokoka lakini hawajaokoka kiukweli, ni kama "kusanyiko la watu mchanganyiko" ambalo liliondoka Misri wakati ule wa Kutoka [angali **Kut 12:38**].) Fungu la maneno katika **mst.20** ya kwamba kumgeuza mwenye dhambi kutoka katika upotevu wa njia yake *"ataokoa roho yake na mauti"* huonyesha kwamba mtu huyu si mwamini wa kweli. Kwa namna yeyote ile, hata hivyo, waamini wanapaswa kuiangalia hali ya afya ya kiroho ya wadada na wakaka kwa raghba ndani ya kanisa na kufanya kila wawezalo kuwaweka katika njia sahihi. Ili waweze kufanya hili, waamini inabidi wajuane vizuri na wawe katika mahusiano ya karibu wao kwa wao. Swala hili kiasili linapaswa kuufuata ule ukweli kwamba kanisa ni familia (**Math 12:49-50; 2 Kor 6:18; Efe 2:19; Gal 6:10; 1 Tim 3:15; 5:1-2; 1 Pet 4:17**). Dhati Lewis anaiweka hivi, "Kanisa si *kama* familia; *ni* familia. . . . Hili linaweza kuonekana kwa ukweli kwamba neno *mwanafunzi*, ambalo lilienea sana wakati wa mwanzo wa Agano Jipya, linapotea baada ya kitabu cha Matendo ya Mitume. Nafasi yake inachukuliwa na neno *ndugu* katika sehemu yote ya Biblia iliyobakia." (Lewis 2015: n.p.) Familia zinahudumiana. Kama Wayne Grudem anavyoonyesha, "Ukweli kwamba kanisa ni kama familia utufanye upendo wetu na ushirika kati yetu kuongezeka" (Grudem 1994: 859). Kwa upande mwingine, ikiwa makanisa hayaanzi kuwatendea washirika wake kama washirika wapendwa wa familia moja, basi dunia

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

(italidhihaki) kihalali kanisa na kuuliza: "Ni kwa nini tuwe Wakristo, wakati ninyi Wakristo wenyewe hampendani?"

Nasaha za Yakobo kwetu anapofunga waraka huu ni muhimu—lakini lile hitaji la kuwarejesha watu kutoka katika upotevu wa njia zao halitakuwa na uwezekano wa kutokea ikiwa kanisa litatilia maanani yale Maandiko yasemayo "sisi kwa sisi" ambayo yamerudiwa mara nyingi. AJ kwa kurudiarudia linawasihi waamini kupendana (**Yohana 13:34-35; Rum 13:8; 1 Thes 3:12; 4:9; 1 Pet 3:8; 4:8; 1 Yohana 3:11, 23; 4:7, 11-12; 2 Yohana 5**), kutiana moyo (**1 Thes 4:18; 5:11; Ebr 3:13; 10:24-25**), kufundishana na kuonyana (**Rum 15:14; Col 3:16**), kuhudumiana (**Yohana 13:14-15; Gal 5:13; 1 Pet 4:10**), kuvumiliana, kuchukuliana, na kukubaliana (**Rum 15:7; Efe 4:2**), kuwa wapole, wenye huruma, wakarimu na wenye kujaliana (**1 Kor 12:25; Efe 4:32; 1 Pet 4:9**), kuishi kwa mwafaka na amani wao kwa wao (**Marko 9:50; Rum 12:16; 1 Pet 3:8**), na kuheshimiana kwa kuwaona wenzitu kuwa ni bora kuliko sisi wenyewe (**Rum 12:10; Fil 2:3**). Kwa kifupi, waaminio *"Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi"* (**Rum 12:10**). Mambo haya yote ni ishara za familia nzuri inayokwenda sawa sawa. Hii ni huduma; ni maisha katika Roho; hivi ndivyo ambavyo maisha katika mwili yanapaswa kuwa. Mstari mwisho wa Yakobo, ya kwamba kumrejeza kaka au dada aliyepotea "*kutafunika wingi wa dhambi,"* ni matumizi yaliyo bayana ya kile ambacho Petro alikisema, *"Zaidi ya yote iweni na juhudi nyingi katika kupendana; kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi"* (**1 Pet 4:8**). Hili na lifanyike katika makanisa yetu.

## MASWALI YA KUJADILI

1. Hii sehemu ya mwisho ya Yakobo inaanza kwa kusema kwamba "kuja kwa Bwana kuko karibu" (Yak 5:8). Ni rai gani ambayo Yakobo anatupa kuhusu jinsi tunavyopaswa kuishi tukiwa tunaelewa kwamba Yesu anakuja tena?

2. Yakobo anakazia kuwa "na subira." Tunawezaje kujifunza subira, na je, kuna jambo lolote ambalo kanisa linaweza kufanya ili kuwasaidia watu wake kuwa watu wa subira?

3. Yak 5:12 inasisitiza kwamba Wakristo—zaidi ya mtu mwingine awaye yote duniani—wanapaswa kuwa watu wa kweli na uadilifu. Tunawezaje kuwa watu ambao tuna sifa ya kuwa wakweli na waadilifu, na je, kuna mambo yoyote ambayo kanisa linaweza na linapaswa kufanya ili kuwasaidia watu wake wawe watu wa kweli na uadilifu?

4. Yak 5:13-18 inasema kuhusu maombi. Ni mambo gani ambayo ni muhimu zaidi ambayo Yakobo anatuarifu kuhusiana na maombi katika kifungu hiki?

5. Katika Yak 5:16 Yakobo anatuambia "ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi."
- Unafikiri ni kwa nini Yakobo anatuambia tuungame dhambi zetu sisi kwa sisi badala ya kuungama dhambi zetu kwa Mungu?
- Ja unafikiri Wakristo wengi wanaungama dhambi wao kwa wao au hapana? Kama hapana, basin i kwa nini?
- Kuungama dhambi zako kwa mtu mwingine humaanisha kwamba una uhusiano na mtu huyo ambao ni wa karibu sana kiasi kwamba unaweza usiohofie usalama wako kwa mtu yule, unaweza kuweka wazi makosa yako, madhaifu na dhambi kwa mtu huyo, na unajua kwamba mtu huyo hatakusaliti. Je, unafikiri kwamba Wakristo wengi wana mahusiano ya namna hiyo na mtu mwingine na, kama sivyo, ni kwa nini sivyo? Nini kinaweza au kinapaswa kufanyika ili kuweza kujenga uhusiano wa aina hiyo ili tuweza kufanya kile ambacho Yakobo anaamuru tukifanye?

6. Kitabu kinamalizika kwa kuzungumza kuhusu kumrejeza mtu ambaye ametoka katika kweli arudi katika njia iliyo sawa.
- Nini kinahitajika ili uweze kufanya hilo?
- Kanisa linawezaje kuwasaidia watu wake waweze kuwasaidia watu wengine warudi katika kweli na kuwezesha ule mchakato wa urejesho?

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

## BIBLIOGRAFIA

*Africa Study Bible, New Living Translation.* 2016. Wheaton, IL: Tyndale House.

Andria, Solomon. 2006. "James." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1509-16. Nairobi: WordAlive.

Augustine. 1950 (reprint). *The City of God.* New York: Random House. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/schaff/npnf102.iv.html.

Bonhoeffer, Dietrich. 1954. *Life Together.* Translated by John Doberstein. New York: Harper & Row. Online: bearsfc.tistory.com/attachment/cfile26.uf@213C214854ADB05A0CCBE3.pdf.

Burdick, Donald. 1981. "James." In *The Expositor's Bible Commentary,* ed. Frank Gaebelein, 159-205. Grand Rapids: Zondervan.

Calvin, John. 1547. *Acts of the Council of Trent with the Antidote*. Online: http://www.monergism.com/thethreshold/sdg/calvin_trentantidote.html.

Carson, D. A., and Douglas Moo. 2005. *An Introduction to the New Testament.* Grand Rapids: Zondervan.

Cole, Victor Babajide. 2006. "Mark." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1171-1202. Nairobi: WordAlive.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature*. Chicago: The University of Chicago Press.

Datiri, Dachollom. 2006. "1 Corinthians." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1377-98. Nairobi: WordAlive.

Davids, Peter. 1982. *The Epistle of James* (NIGTC). Grand Rapids: Eerdmans.

Dostoevsky, Fyodor. 1957. *The Brothers Karamazov*. Translated by Constance Garnett. New York: New American Library. Online (another edition): http://pinkmonkey.com/dl/library1/book0664.pdf.

*Epitome of the Formula of Concord.* 1577. Online: http://bookofconcord.org/fc-ep.

Eusebius. 1988 (reprint). *The Ecclesiastical History of Eusebius Pamphilus.* Grand Rapids: Baker. Online: http://www.ccel.org/ccel/schaff/npnf201.toc.html.

Fee, Gordon. 1984. "The 'Gospel' of Prosperity—an Alien Gospel." *Reformation Today* 82: 39-43.

France, R. T. 1992. "Faith." In *Dictionary of Jesus and the Gospels,* ed. Joel Green, Scot McKnight, and I. Howard Marshall, 223-26. Downers Grove, IL: InterVarsity.

Grudem, Wayne. 1994. *Systematic Theology.* Grand Rapids: Zondervan. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0310286700.

Hoekema, Anthony. 1979. *The Bible and the Future.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Johnson, Luke Timothy. 1995. *The Letter of James* (AB 37A). New York: Doubleday.

Josephus. 1987. *The Antiquities of the Jews.* In *The Works of Josephus Complete and Unabridged.,* 27-542. Translated by William Whiston. Peabody, MA: Hendrickson. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/josephus/works/files/works.html.

Lewis, Dhati. 2015. "The Church Is Not Like A Family." Online: http://www.vergenetwork.org/2017/03/14/the-church-is-not-like-family/?inf_contact_key=563a07f48051945f93bdc050b4bbef102519cd85d688856b793a9898205d2ff9.

*Life Application Study Bible, New International Version.* 1986. Wheaton, IL: Tyndale House.

Lindsell, Harold. 1971. "Introduction to the Letter of James." In *Harper Study Bible, Revised Standard Version,* 1822-23. Grand Rapids: Zondervan.

Copyright © by Jonathan Menn 2019. All rights reserved.

Luther, Martin. 1535. *A Commentary on St. Paul's Epistle to the Galatians.* Translated and abridged by Theodore Graebner. Online: http://www.ccel.org/ccel/luther/galatians.i.html.

Marshall, I. Howard, Stephen Travis, and Ian Paul. 2002. *Exploring the New Testament: A Guide to the Letters and Revelation.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Martin, Ralph. 1988. *James* (WBC 48). Waco, TX: Word.

Menn, Jonathan. 2016. *Biblical Theology.* Online: http://www.eclea.net/courses.html#theology.

Moo, Douglas. 1985. *James* (TNTC). Grand Rapids: Eerdmans.

_______. 1989. "James." In *Evangelical Commentary on the Bible,* ed. Walter Elwell, 1150-62. Grand Rapids: Baker.

*New American Standard Bible.* 1995. Grand Rapids: Zondervan.

Ngundu, Onesimus. 2006. "Revelation." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1543-79. Nairobi: WordAlive.

Nystrom, David. 1997. *James* (NIVAC). Grand Rapids: Zondervan.

Sarles, Ken. 1986. "A Theological Evaluation of the Prosperity Gospel." *Bibliotheca Sacra* 143: 329-52.

Schowalter, Daniel. 1993. "Faith." In *The Oxford Companion to the Bible,* ed. Bruce Metzger and Michael Coogan, 222-23. New York: Oxford University Press.

Tasker, R. V. G. 1982. *The General Epistle of James* (TNTC). Grand Rapids: Eerdmans.

Travis, Stephen. 1982. *I Believe in the Second Coming of Jesus.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Ward, Ronald. 1970. "James." In *New Bible Commentary,* 3rd ed., ed. D. Guthrie and J. A. Motyer, 1222-35. Carmel, NY: Guideposts.

Zodhiates, Spiros. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament,* rev. ed. Chattanooga, TN: AMG.

## MWANDISHI



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipata B.A. yake katika Sayansi ya Siasa kutoka Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, na kuibuka na daraja la juu la heshima, mwaka 1974, na kuingizwa katika jamii inayoheshimika ya Phi Beta Kappa. Kisha akapokea J.D. kutoka Cornell Law School, magna cum laude, mwaka 1977, na akawa miongoni mwa Jamii ya Sheria inayoeshimika ya Coif. Alitumia miaka 28 inayofuata akijihusisha na shughuli za sheria, kama wakili wa sheria anayejitegemea kule Chicago na baadaye kama mdau Kitengo cha sheria cha Menn Law Firm kule Appleton, WI. Mwaka 1982 akaamini na kuwa mfuasi wa Yesu Kristo. Upendo wake unaokua katika theolojia unalimfanya ahitimu shahada yake ya pili katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School kule Deerfield, IL. Akahitimu shahada ya pili ya theolojia kutoka TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya 2007-2013 alikuwa Mkurugenzi wa Equipping Pastors International. Sasa Jonathan ni Mkurugenzi wa Equipping Church Leaders-East Africa (**www.eclea.net**). Machapisho yake yaliyosheheni ya masomo ya Biblia yanapatatikana kwenye **www.eclea.net.** Jonathan anaweza kuandikiwa au kuwasilana naye kupitia barua pepe hii: **jonathanmenn@yahoo.com**.